# Nipashe

Jumatano Agosti 12, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580308

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Serikali sasa yapiga marufuku mtoto kusafirishwa bila kibali

UKURASA 3



Wanasiasa wasiowajibika walivyochokwa Pemba

Ukurasa 13

siasa

JUMATANO JAGOSTI 12, 2020 Nipashe HABARI BORA NA KAMILIFU

Ukurasa 14

KENETH KAUNDA: Mkombozi pekee anayeishi Afrika Mkapa alisaidia kumtoa gerezani

Mkapa alikuwa mwanastratejia hodari na muumini halisi wa Nyerere

- Mwalimu hakumpendelea Ben 1995
- Kampeni yetu haikumwogopa Mrema
- Hakuna njia ya kutomteua JK kuwa Waziri
- Hakuniteua kuwa meneja wa kampeni

Na Waandishi Maalum

UKURASA 11

# Kauli mpya ya IGP kwa Lissu

**NI** kuhusu uchunguzi shambulio la risasi, aonya wanasiasa kuelekea uchaguzi mkuu... *Endelea ukurasa wa 2*




Mgombea Urais wa CCK, David Daudi Mwaijojele




Mgombea Urais wa CUF, Prof. Ibrahim Lipumba




Mgombea Urais wa NCCR Mageuzi, Yeremia Kulwa Maganja




Mgombea Urais wa ADA TADEA, John Shibuda

## Wanne zaidi wajitosa urais

UKURASA 4




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## SOPHIA SIMBA APETA KURA ZA WAJUMBE UBUNGE CCM

UKURASA 2

MICHEZO ZAHERA RASMI MKURUGENZI WA UFUNDI GWAMBINA FC UK.23

MAONI, KATUNI UK.6

# Kauli mpya ya IGP kwa Lissu

**Na Salome Kitomari**

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP), Simon Sirro, amewaonya wanasiasa walioanza kuonyesha shari kupitia matamshi na sura zao kuelekea uchaguzi mkuu.

Sirro pia amezungumzia maendeleo ya uchunguzi wa jeshi hilo kuhusu shambulio la kupigwa risasi kwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu.

IGP Sirro alizungumzia masuala hayo juzi wakati akihojiwa kwenye kipindi cha Dakika 45 kinachorushwa na kituo cha luninga cha ITV.

Kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi aliwataka wanasiasa kutolichokoza jeshi hilo na pia wasililaumu litakapochukua hatua dhidi yao.

"Nimeona viongozi wa siasa wanazungumza mambo makali sana. Ninawaheshimu viongozi wote wa siasa katika ngazi zote lakini lazima sheria na kanuni zilizopo ziheshimiwe.

"Ukiangalia baadhi ya viongozi wanavyozungumza unaona kuna ushari. Ushari wanaonyesha wanaupeleka kwa washabiki wao wawe na ushari huo huo. Wao wanachozungumzia si uchaguzi wa amani na utulivu, sera yao ni ushari," alisema bila kutaja viongozi wala chama cha siasa.

"Niwaombe sana (viongozi wa siasa) anayetaka kufanya siasa afanye siasa, anayetaka kufanya ushari aache mapema. Unamkuta kiongozi mkubwa anazungumza maneno ya ukali sana, anasahau amepata nafasi ya kuzungumza kutokana na amani iliyopo. Kama siyo amani angekuwa chini ya uvungu wa kitanda chake.

"Sheria na taratibu zimewekwa na NEC (Tume ya Taifa ya Uchaguzi), habari ya kusema nimeshazungumza nimemaliza basi hakuna wa kuhoji (anamrejelea kiongozi anayezungumza kwa shari), hii siyo lugha nzuri. Watanzania wengi wanapenda amani, hawataki shida...lakini wakumbuke kuna maisha baada ya uchaguzi. Uchaguzi utapita na tutaendelea kuishi tuna watoto na wajukuu, tunataka amani na utulivu," alisisitiza.

Kwa mujibu wa IGP Sirro, viongozi wanaoanza na ushari wasilaumu vyombo vya dola kwa kuwa Watanzania wanaona kuna jambo wanalitafuta la ushari.

"Kwa kuwa nina dhamana ya ulinzi na usalama, wanaojiandaa kwa ushari wajue sisi tupo kwa mujibu wa sheria, na wanaoz-ivunja sheria, tukianza kuwashughulikia asitulaumu," alisema.

Sambamba na hilo, IGP alibainisha kwa Tanzania haiwezi kupata viongozi wazuri katika vurugu bali watapatikana kukiwa na amani tele na kwamba ni vyema viongozi hao wakaendelea kunadi sera zao kuliko kutafuta shari.

Aidha, aliwataka vijana kutojiingiza kwenye mambo yanayofanywa (shari) kwa maslahi ya wachache, na kwamba ni vyema wakaangalia familia zao na maisha kwa ujumla.

# Sophia Simba apeta ubunge CCM

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Wanawake ya CCM (UWT) na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM aliyefukuzwa uanachama na baadaye kurejea tena, Sophia Simba, ameonyesha kurejea tena katika duru za siasa nchini baada ya kupenya kwenye tatu bora za kuwania ubunge wa viti maalum.

Juzi, Sophia (pichani) katika kura za maoni za kuwasaka wabunge wa viti maalum kuwakilisha taasisi zisizo za kiserikali (NGOs), alishika nafasi ya tatu baada ya kupata kura 43.

Kundi hilo lilikuwa na wagombea 21 na nafasi zilizokuwa zikiwaniwa ni tatu, Neema Lugangila akiongoza kwa kura 60 akifuatwa na aliyewahi kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Rita Mlaki, aliyepata kura 48.

Kundi la vyuo vikuu, wagombea 21 walipigiwa kura za maoni kuwania nafasi tatu. Msimamizi Mkuu wa Uchaguzi huo, Salum Khatib Reja, alimtangaza Paulina Nahato kuongoza kwa kura 75, akifuatwa na Aziza Msuya (70) na Thea Ntara (44).

Katika kundi la watu wenye ulemavu, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Watu Wenye Ulemavu), Stella Ikupa, aliongoza kwa



kupata kura 94 akifuatwa na Khadija Taya (39) na Ummy Ndeliyananga (38).

Wagombea 23 walijitosa kuwania ubunge wa viti maalum kupitia kundi la vyama vya wafanyakazi, Alice Kaijage akioongoza kwa kura 77, akifuatwa na Jenejeri Ntate (32) na Lucy Mwakyembe (28).

Kwa upande wa viti maalum kupitia kundi la vyuo vikuu katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar, walioongoza kura za maoni ni Mariam Khamis (103), Saada Ramadhan (86) na Riziki Juma (59).

Vilevile, katika kuwania ubunge wa viti maalum kupitia kundi la watu wenye ulemavu katika baraza hilo, walioongoza kura za maoni ni Mwantatu Khamis aliyepigiwa kura 122, akifuatwa na Zainab Salum (55) na Fatma Shaibu (46).


bgtl BEST GROUP (T) LIMITED
Debts collector, Auctioneer, Commission Agent, Broker & Legal Consultant

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa Idhini tuliyopewa na **BANK OF AFRICA (BOA)** tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana ya mdaiwa tajwa hapo chini, mahali dhamana ilipo kama inavyooneshwa katika jedwali hapo chini ;Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 asubuhi na kuendelea

| Na. | JINA LA MDAIWA | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | **BEATUS ASSEY/ALBINA TESHA** | Kiwanja na.5, kitalu "S" Ofisi ya ardhi namba 351152 chenye ukubwa wa mita za mraba 1002 (sqm) chenye jina la **ALBINA JOHN TESHA** kilichopo maeneo ya Goba Tegeta manispaa ya Kinondoni | 05/09/2020 |

**MASHART YA MNADA**
1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2.Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**

**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**Bank of Africa**
**Head Office,**
**NDC Development House, ohio street-kivukoni**
**P.O.BOX 3054,**
**DAR ES SALAAM**
**Tel:+255 -22-2110104/2111290**
**Fax: +255-22-2113740**

115854802


# Bei nafuu elekezi ya mbolea yatangazwa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, ametangaza bei elekezi ya mbolea ya kupandia (DAP) na kukuzia (Urea) kwa msimu wa mwaka 2020/21, huku ikiwa imeshuka ikilinganishwa na msimu uliopita.

Hasunga akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, alisema bei ya mbolea msimu wa 2020/21 imepungua kwa wastani wa Sh.1,316 kwa mfuko wa kilo 50 wa UREA ikilinganishwa na msimu wa 2019/20.

Aidha, alisema kwa DAP bei imepungua kwa wastani wa Sh. 2,860 kwa mfuko wa kilo 50 ikilinganishwa na msimu wa 2019/20.

Alisema faida nyingine ni kwamba, mbolea iliyoagizwa na vyama vya ushirika imewafikia wanachama wao mpaka vijijini walipo.

"Wastani wa bei ya mbolea ya DAP kitaifa kuanzia leo (jana) kwa msimu wa 2020/21 itakuwa Sh. 55,573 kwa mfuko wa kilo 50 ikilinganishwa na Sh. 58,433 kwa mfuko wa kilo 50 msimu wa 2019/20," alisema.

Kwa upande wa mbolea ya UREA, alisema wastani wa bei kitaifa kwa msimu wa 2020/21 itakuwa Sh. 48,070 kwa mfuko wa kilo 50 ikilinganishwa na Sh. 49,386 msimu wa 2019/20.

Alibainisha kuwa mchanganuo wa bei elekezi za mbolea ya DAP na UREA kwa mkoa mmoja na mwingine zinatofautiana kutokana na umbali kutoka Dar es Salaam, hali ya barabara na gharama za usafiri.

Akizungumzia ulinganifu wa bei elekezi za msimu wa kilimo 2019/20 na 2020/21 kwa mfuko wa mbolea ya DAP kilo 50 kimkoa, alitolea mfano kuwa Arusha ni Sh. 55,356 (2020/21) ikilinganishwa na Sh. 58,208 (2019/20), Dodoma Sh. 53,925 (2020/21) ikilinganishwa na Sh. 56,790 (2019/20).

Aidha, mkoa wa Dar es Salaam Sh. 48,717 (2020/21) ikilinganishwa na Sh. 51,925 (2019/20), Geita 58,313 (2020/21) ikilinganishwa na Sh. 61,138 (2019/20), Iringa Sh. 54,563 (2020/21) ikilinganishwa na Sh. 57,422 (2019/20).

Pia, Kagera Sh. 59,195(2020/21) ikilinganishwa na Sh. 62,011 (2019/20), Katavi Sh. 59,431 (2020/21) ikilinganishwa na Sh. 62,246 (2019/20), Lindi Sh. 54,043 (2020/21) ikilinganishwa na Sh. 56907(2019/20).

Manyara Sh. 56,460 (2020/21) ikilinganishwa na Sh. 59,302 (2019/20), Mara Sh. 59,327(2020/21) ikilinganishwa na Sh. 62,142(2019/20), Mtwara Sh. 54,780 (2020/21) ikilinganishwa na Sh. 57,637 (2019/20), Rukwa Sh. 59,255 (2020/21) ikilinganishwa na Sh. 62,072 (2019/20).

Shinyanga ni Sh. 57533(2020/21) ikilinganishwa na Sh.60,365 (2029/20), Songwe Sh. 57,480 (2020/21) ikilinganishwa na Sh. 60313 (2019/20), huku Simiyu ikiwa ni Sh. 57,544 (2020/21) ikilinganishwa na Sh. 60,376 (2019/20).

Alisema Bei elekezi kwa mbolea zilizoingizwa na vyama vya ushirika kwa msimu wa 2020/21 zitakuwa Sh. 50,000 kwa mfuko wa kilo 50 wa DAP na Sh. 43,500 kwa mfuko wa kilo 50 wa mbolea aina ya UREA.

## HABARI KITAIFA



Daktari kutoka hospitali ya rufani ya Mkoa Shinyanga, Onesmo Mwigoha, akitoa elimu kwa waandishi wa habari mkoani Shinyanga jana, kuhusu namna ya kuandika habari za kinga na kutokomeza magonjwa ya mlipuko ndani ya jamii, kikiwamo kipindupindu na maambukizi ya virusi vya Corona. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Maelfu wawapokea Membe na Maalim Seif Pemba

**Na Romana Mallya**

MAELFU ya wanachama na wafuasi wa chama cha ACT-Wazalendo, wamejitokeza visiwani Pemba katika mkutano wa kuwapokea wagombea urais kupitia chama hicho, Maalim Seif Sharif Hamad (Zanzibar) na Bernard Membe (Tanzania).

Jana, wagombea hao walifika kisiwani huko kwa lengo la kuwashukuru wanachama wao.

Akizungumza katika mkutano huo, Maalim Seif alilitaka Jeshi la Polisi kuepuka kutumika kisiasa kuelekea uchaguzi mkuu uliopangwa kufanyika Oktoba 28 mwaka huu.

Maalim Seif pia aliwataka wanachama wa ACT-Wazalendo kutokubali kuchanganywa na watu wenye tamaa.

"Twende kwenye tulilokusudia kukomboa nchi yetu, mmepiga kura ya maoni, chama kitayaheshimu na nitoe onyo mtu yeyote atakayekula rushwa tutamkata.

"Wasipite mtaani wakawachanganya hatukufanya kwa siri, tulipita kila jimbo kuwaambia wengine wakajifanya hodari wana fedha, msimamo wa mwenyekiti wa chama mtoa rushwa anakatwa.

"Mnamtaka waziri mla rushwa? Mnamtaka mkuu wa mkoa mla rushwa? Tukiwarudisha watoa rushwa, tutakuwa watoa rushwa katika nchi, tunachotaka ni kuipata nchi," alisema.

Mgombea wa urais wa chama hicho Tanzania, Membe, aliwaahidi Wazanzibar kuwa atahakikisha wanapata haki zao.

# Serikali sasa yapiga marufuku mtoto kusafirishwa bila kibali

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, ameviagiza vyombo vya ulinzi na usalama nchini, kuhakikisha kila mtoto mwenye umri wa chini ya miaka 18, anayesafirishwa kutoka eneo moja kwenda jingine anakuwa na kibali cha mzazi na kile cha kiongozi wa serikali za mitaa.

Pia, amemwagiza katibu mkuu wa Wizara yake, kuwasiliana na Wizara ya Mambo ya Nje, ili kuwabaini na kuwarejesha nchini Watanzania wote waliopo nje ya nchi ambao wanadaiwa kufanyiwa vitendo vya ukatili, unyanyasaji na kutumikishwa.

Simbachawene aliyasema hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akifungua maadhimisho ya kitaifa kupinga biashara haramu ya kusafirisha binadamu.

Alisema hivi sasa nchini hali ni mbaya hasa katika maeneo ya miji mikubwa ambapo biashara ya kusafirisha watu imeshamiri hasa kwa wanawake na watoto wa kike.

Alisema kutokana na hali hiyo, vyombo vya ulinzi katika Wizara yake vinatakiwa kufanya kazi ya ziada ili kukabiliana na biashara hiyo haramu ya kusafirisha binadamu.

Alisema vyombo vya ulinzi vinatakiwa kuacha kufanya kazi kwa mazoea kama ilivyozoeleka bali vinatakiwa kutimiza majukumu yao kwa vitendo.

"Biashara hii hata hapa tukisema tutoke twende kwenye mabasi barabarani tukafanye ukaguzi kwenye mabasi lazima tutawakuta watoto watatu hadi wanne, ambao wanasafirishwa bila wao kujua kule wanakokwenda wanakwenda kufanya nini,"alisema Simbachawene.

Waziri huyo alisema kutokana na hali hiyo, vyombo vya ulinzi vinatakiwa kuacha kufanya kazi kwa nadharia bali viendeshe misako mikali katika magari mbalimbali ili kukomesha biashara hiyo haramu.

Vile vile, alisema pamekuwapo na watu ambao ni maarufu kwa kukusanya watoto kutoka katika mikoa mbalimbali na kwenda kuwauza kwa watu wanaohitaji wasichana wa kazi.

Aliwaonya Watanzania kutotumia kigezo cha umasikini na ukosefu wa ajira nchini kama kichocheo cha kuruhusu kirahisi vijana na mabinti kwenda nje ya nchi kwa sababu ya kutafuta kazi, ambapo alisema ni vyema kutumia fursa na rasilimali zilizopo kujikwamua.

Alisema, wengi husafirishwa kutoka Tanzania kwenda nje ya nchi, baada ya kufika huko wanajikuta wanaishia kutumikishwa katika biashara ya ukahaba hususani katika nchi za India, Thailand, China, Indonesia na Malasya.

Alisema kuwa, wengine wanatumikishwa kwa kazi za ndani katika nchi za Oman na baadhi ya nchi nyingine za uarabuni ikiwemo Iraq.

Alieleza kuwa, wahanga wengi wanaosafirishwa nje ya nchi wanatokea jijini Dar es Salaam, Tanga na Dodoma (Hususani Wilaya ya Kondoa) na wachache ni kutoka mikoa mingine na waathirika wakubwa ni wanawake kuanzia umri wa miaka 16 hadi 26.

Mkuu wa shirika la kimataifa linalojihusisha na masuala ya uhamaji (IOM), Dk. Qasim Sufi, alisema, huu ni mwaka wa 20, wanafanya maadhimisho ya kupinga biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya kitaifa ya kuzuia na kupambana na biashara haramu ya kusafirisha binadamu, Adatus Magere, alisema biashara hiyo ina mtandao mkubwa kimataifa na kitaifa.

Alisema kuwa biashara hiyo inahusisha magenge ya kimataifa yanayojihusisha na uharifu, na wakati mwingine inahusisha wafanyabiashara wa dawa za kulevya.


CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA VIWANDA, BIASHARA, TAASISI ZA FEDHA, HUDUMA NA USHAURI (TUICO)

**TANGAZO LA RATIBA YA UCHAGUZI MKUU WA TUICO KWA MWAKA 2020**

A. Kwa mujibu wa Katiba ya Chama ya mwaka 1995, Rekebisho la Tano (2015); Sura ya 6 na 14 zikisomwa pamoja na Kanuni za Katiba ya Chama, Kanuni ya 17; taarifa hii inatolewa kwa Wanachama wote wa TUICO kuwa Ratiba ya Uchaguzi Mkuu wa Chama mwaka 2020 Ngazi ya Mkoa, Kanda na Taifa iliyopitishwa na Baraza Kuu mwezi Mei, 2020 ni kama ifuatavyo:-

**1. NGAZI YA MKOA**

Uchaguzi wa viongozi Ngazi ya Mkoa, Kamati za Wanawake na Wawakilishi wa Vijana utafanyika mwezi Septemba, 2020. Nafasi zitakazogombewa ni kwa mujibu wa Katiba kama ifuatavyo:-

(a) Sura ya Nane, Kipengele cha 8.2.3.2
(b) Sura ya Kumi na Nne, Kipengele cha 14.1.9

**2. NGAZI YA KANDA**

Uchaguzi wa Viongozi Ngazi ya Kanda utafanyika mwezi Novemba, 2020.

**3. NGAZI YA TAIFA**

Uchaguzi wa Viongozi Ngazi ya Taifa, Kamati ya Wanawake Taifa na Kamati ya Vijana Taifa, utafanyika mwezi Desemba, 2020.

**B. FOMU ZA KUGOMEBA UONGOZI:**

Fomu za kugombea nafasi za uongozi zilizotajwa katika sehemu (A) zitapatikana Ofisi za TUICO mikoa yote. Wakati wa kuchukua fomu ni lazima uoneshe nyaraka zifuatazo:-

(i) Kadi ya Uanachama
(ii) Nakala kivuli ya "Salary Slip" au uthibitisho mwingine wa malipo ya ada ya Chama.

**C. KUCHUKUA NA KUREJESHA FOMU UCHAGUZI MKUU NGAZI YA MKOA**

Zoezi la kuchukua fomu za kugombea uongozi kwenye Uchaguzi Mkuu Ngazi ya Mkoa litaanza tarehe 17 Agosti, 2020. Siku ya mwisho ya kurejesha fomu ni tarehe 31 Agosti, 2020 Saa Kumi Kamili Jioni (10:00). Hakikisha fomu yako unamkabidhi Katibu wa TUICO mkoa husika.

**D. SIFA ZA WAGOMBEA:**

1. Awe Mwanachama hai kwa mujibu wa Katiba ya Chama na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 ambaye analipa michango yake ya kila mwezi kwa wakati unaotakiwa.
2. Awe anajua kusoma na kuandika kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza.
3. Awe anazingatia Katiba na Kanuni za Chama na kuheshimu maamuzi yatokanayo na vikao.
4. Awe na uelewa wa masuala ya Vyama vya Wafanyakazi na aweze kutetea Sera za Chama chake wakati wote.
5. Awe anaunga mkono na kusaidia kwa vitendo maendeleo ya Chama.
6. Awe mfano mzuri wa utendaji kazi na mwenye bidii ya kazi.
7. Mgombea wa uongozi nafasi ya vijana awe na umri kuanzia miaka 15 hadi 30
8. Awe jasiri na mvumilivu katika kusimamia na kutekeleza maamuzi ya Chama na kutetea haki, heshima na maslahi ya Wanachama.
9. Awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai na kuhukumiwa.
10. Awe hajawahi kufukuzwa uanachama au kuondolewa katika uongozi wa Chama.
11. Awe makini katika kutoa maamuzi ya Chama.

**E. WITO KWA WANACHAMA WOTE**

Wanachama wote hasa wanawake na vijana mnahamasishwa kujitokeza kuchukua fomu za kugombea uongozi katika ngazi mbalimbali zilizotajwa hapo juu ili kukuza na kuimarisha demokrasia ndani ya Chama.

**F. MWISHO**

Chama kinawatakia heri ya maandalizi na mafanikio mema katika uchaguzi huu wa mwaka 2020.

**MSHIKAMANO DAIMA!**

B.Y. Nkakatisi
KATIBU MKUU TUICO

215853602



Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo (aliyevaa hijjab ya bluu), akikagua eneo ambalo limetengwa kwa ajili ya ujenzi wa msikiti wa Wilaya ya Kisarawe, mkoani Pwani juzi, shughuli ambayo ameahidi kuisimamia kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje ili ndani ya mwaka mmoja ujenzi huo uwe umekamilika. Wengine ni viongozi na waumini wa dini hiyo. **PICHA: ROMANA MALLYA**

# Wanne zaidi wajitosa urais

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAGOMBEA urais wanne kutoka vyama mbalimbali vya siasa, wamejitokeza kuchukua fomu ya kuomba kuteuliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi(NEC) kuwania nafasi hiyo kwenye Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu na kufikisha idadi ya wagombea 16.

Uchukuaji fomu hizo ulianza Agosti 5 na utahitimishwa Agosti 25, mwaka huu, ambapo wagombea hao wamekuwa wakitoa sera zao kwa Watanzania, huku wengine wakiingia katika ofisi hizo kwa vituko mbalimbali.

Jana wagombea waliojitokeza ni pamoja na wa CCK, David Maijojele , Mgombea wa CUF, Prof.Ibrahim Lipumba, Mgombea Chama cha NCCR-Mageuzi, Yeremia Maganja, Mgombea wa chama cha ADA TADEA, John Shibuda.

**LIPUMBA ATINGA NA MATARUMBETA**

Prof. Lipumba akiwa na Mgombea mwenza wake Hamida Abdallah Huweishi, viongozi na wanachama wa chama hicho walitinga ofisi ya NEC wakiwa na matarumbeta huku akisema hiyo ni sherehe sio msiba.

Akizungumza mara baada ya kuchukua fomu, mgombea huyo alisema chama hicho msingi wake ni haki sawa na furaha kwa wote huku akisema chama hicho kitaweka grisi ili vyuma visikaze.

"Madhumuni yetu sisi ya kugombea urais na ikiwa tutapata fursa hiyo na Watanzania watatuchagua, jambo la kwanza tutaunda serikali ya umoja wa kitaifa, tunahitaji kufanya hivyo ili lile zoezi la kupata Katiba yenye msingi mizuri ya kidemokrasia iweze kufanikiwa, na kama Taifa tuwe na dira ya pamoja ambapo vyama vyote vitaitazama dira hiyo kuongoza Taifa," alisema.

Aidha alisema katika malengo ya kidunia ya kutokomeza umaskini katika nyanja zote ifikapo mwaka 2030, chama hicho kimejikita kujenga uchumi unaokua kwa kasi na kuongeza ajira.

"Vijana hivi sasa wameanzisha msamiati mpya kwamba vyuma vimekaza, sera za kuwekea grisi vyuma vilivyokaza ni sera za haki sawa kwa wote, tutaongeza mzunguko wa fedha na tutahakikisha shughuli za biashara, uwekezaji zinakuwa nyepesi kuliko ilivyo hivi sasa," alisema.

Prof.Lipumba alisema "Ukitazama kipindi cha miaka mitano hata kampuni mpya zilizosajiliwa nchini Tanzania mwaka 2015 zilikuwa 8,800, mwaka 2019 zimepungua mpaka kufikia kampuni 6,000 kwasababu mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji yamekuwa magumu."

Alisema watajenga mazingira hayo mazuri ya uwekezaji.

Jambo jingine, alisema ni kuwa na elimu bora ili kutokomeza umaskini.

**MGOMBEA CCK KUPAISHA KILIMO**

Mgombea wa CCK, David Maijojele, ambaye alifika bila mgombea mwenza wake Ali Saidi Juma, alisema chama hicho kitafanya siasa za kistaarabu, amani, upendo, mshikamano na umoja kwa kuwa ndio tunu za Taifa.

"Kutokana na chama chetu kuwa cha kijamii tunazingatia kuhudumia jamii ambapo tutahakikisha wakulima wanakuwa na kilimo cha kisasa kinachowaletea tija na faida, sisi tukikabidhiwa serikali tutahakikisha mkulima anakuwa na kilimo kinachomletea mafanikio makubwa," alisema.

**MGOMBEA NCCR-MAGEUZI**

Naye, Mgombea wa NCCR-Mageuzi, Yeremia Maganja, ambaye aliambatana na mgombea mwenza, Haji Ambari Hamisi, alisema atahakikisha anasimamia mgawanyo wa madaraka ikiwemo uteuzi wa majaji.

Alisema ataweka utaratibu ambao ni huru kwa wananchi wasiwe na wasiwasi kwenye utendaji haki.

**MGOMBEA WA ADA TADEA**

Mgombea wa ADA TADEA, John Shibuda na mgombea mwenza, Hassan Kijogo, walichukua fomu huku Shibuda akimpongeza Rais John Magufuli kwa kutoa tamko kuwa uchaguzi utakuwa huru na haki na kuhimiza wengine wajitokeze kuwania.

"Kwakuwa Watanzania tupo msimu wa gumzo za kisiasa Nina uhakika baada ya miaka mitano Watanzania watajua pa kurekebisha ili nchi uwe na maendeleo

"Uongozi bora ni ule unaokidhi matakwa na matamanio ya Watanzania, uongozi bora ni ule usio na mgogoro wa afya ya akili hivyo uongozi upo kwenye fumbo la samaki, ikiwa afya ya kiongozi anayeongoza ina matata lazima taifa liwe na matatizo

**KAULI YA NEC**

Mkurugenzi wa Tume hiyo, Dk.Wilson Mahera, alisema kimebaki Chama kimoja Cha NLD ambacho bado hakijafanya uteuzi na kitakapokamilisha uchukuaji fomu utafanyika jijini Dar es salaam.

"Kwa sasa Dodoma tumekamilisha tutarudi tena Agosti 23 hadi 25 ili kutoa majina ya wagombea walioteuliwa, kwasasa wagombea wamechukua fomu na wanazijaza na kutafuta wadhamini," alisema.

## DC Jokate awahakikishia Waislamu msikiti wa kisasa

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo, amewahakikishia Waislamu wilayani humo kuwa ujenzi wa msikiti wa kisasa wa Wilaya wa ghorofa mbili unajengwa kwa sababu huduma ambazo zitatolewa hapo zitasaidia kupambana na umaskini, ujinga na maradhi.

Akizungumza na waumini wa dini hiyo juzi wilayani humo ambao wamemuomba awe mlezi, Mwegelo alisema katika maisha yake hakuwahi kufikiria kupewa heshima kubwa ya ulezi na kuahidi kushiriki kikamilifu katika ujenzi wake.

Ujenzi wa msikiti huo hadi kukamilika kwake utagharimu zaidi ya Sh. milioni 500.

Mwegelo aliahidi kusimamia ujenzi huo unaotarajiwa kukamilika ndani ya mwaka mmoja na kuwaeleza kuwa, anaamini hakuna kitakachoshindikana na tayari ameanza kuzungumza na wadau wa ndani na nje ili kusaidia ujenzi huo.

Alisema msikiti huo utakapokamilika utabeba taswira ya wilaya hiyo ya Kisarawe.

"Katika maisha yangu sijawahi kufikiria kuna siku moja nitapata heshima ya kuwa mlezi wa msikiti na kuombwa kushiriki kikamilifu kwenye ujenzi wa msikiti lakini wananchi wa Kisarawe mmenipa heshima hii ambapo ninaahidi sitawaangusha na nitashirikiana nanyi bega kwa bega hadi msikiti ukamilike," alisema.

Alisema atahakikisha wanafanikisha ujenzi wake ili uwe taswira ya misikiti mingine ndani ya wilayani humo.

"Tunafahamu msikiti ni taasisi inayojishughulisha na mambo mbalimbali ya kimaisha katika jamii ikiwa ni pamoja na shughuli za maendeleo, kiuchumi na kiutamaduni na kwa mantiki hii ni jambo muhimu katika kuratibu utekelezaji wa shughuli hizo, tunaamini

huduma ambazo zitatolewa na msikiti huu zitasaidia katika kupambana na umasikini, ujinga na maradhi na wananchi na taifa kwa ujumla litasonga mbele," alisema.

Alisisitiza kuwa maandiko Matakatifu ya Quraan yanaeleza Mwenyezi Mungu humpenda mja wake anayejituma katika kufanya kazi, hivyo akiwa mlezi wa kamati iliyoundwa kushughulikia ujenzi huo atajitajidi kadri atakavyojaaliwa kutoa mchango wake wa hali na mali kufanikisha ujenzi huo mkubwa na wa kihistoria.

"Sote tunafahamu kwamba tuko kwenye kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba 28, ninatoa rai kwenu, dini zote na wananchi wote kuzingatia amani na utulivu. Sitarajii uvunjifu wa amani ndani ya Wilaya ya Kisarawe.

"Ninasema haya nikiamini viongozi wa dini ndiyo walezi wetu mpo karibu na jamii, tuwasaidie vijana watulie, uchaguzi ufanyike kwa usalama na kisha tuendelee na majukumu yetu ya kuijenga Kisarawe.

Katibu wa msikiti huo , Mohamed Bakari alisema kwamba wazo la ujenzi wake ulianza mwaka 2000 na eneo lilipatikana mwaka 2006 na ilipofika mwaka 2007 wakapata ramani na ujenzi wa msingi ulianza mwaka juzi.

"Tulianza kuchangishana fedha kupitia michango ya waumini wetu na katika kipindi cha miaka 10 tukafanikiwa kukusanya Sh.milioni 45 lakini ili msikiti huu ukamilike kama ramani ilivyo, tunahitaji kupata zaidi ya Sh.milioni 500.

HABARI KITAIFA

# ILO: Yanahitajika maboresho kukabili magonjwa hatarishi

**Na Mwandishi Wetu**

OFISI ya Shirika la Kazi Duniani (ILO), imeishauri Tanzania kuweka kipengele cha mlipuko wa magonjwa hatari ya kuambukiza (pandemic) kwenye sheria ya kazi ili kupunguza athari na changamoto zinazowakumba waajiri na wafanyakazi kutokana na maradhi.

Mratibu wa Programu ya Kitaifa ya Uongozi Bora ya ILO, Maridadi Phanuel, alisema hayo jijini Dar es Salaam kwenye jukwaa la kitaifa la vijana, ajira na kazi zenye staha.

Alisema, taifa lijifunze changamoto za corona na jinsi zilivyoathiri sekta ya ajira na kuweka kipengele cha namna ya kukabiliana na matukio ya magonjwa hatari ya kuambukiza kwenye Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini.

Anawaambia washiriki wa jukwaa hilo lililoandaliwa na shirika la kimataifa la ActionAid, kuwa corona ilileta usumbufu kwa waajiriwa kama kupunguzwa kazi, kukatwa mishahara, likizo bila malipo yote yakifanyika bila majadiliano ya utatu (waajiri, serikali na wafanyakazi).

Alisema, kukiwa na sheria kama hiyo, waajiri, waajiriwa na serikali wakawa pamoja kujadiliana na kufanya uamuzi sahihi, kutapunguza usumbufu kama huo ulioletwa na corona.

Akiwasilisha mada ya umuhimu wa kazi zenye staha, alisema waajiriwa wengi hawakushirikishwa kwenye uamuzi uliofanywa na waajiri wakati wa kuamua hatua za kuchukua kukabiliana na corona.

Phanuel aliwataka waajiri kusimamia na kukubaliana na sheria, sera na taratibu za kazi za ILO zinazowataka kuwa na mikataba ya ajira, kulipa mishahara, kutoa stahili za waajiriwa kama likizo ya uzazi, matibabu na kuwasilisha michango ya akiba za wafanyakazi kwenye mifuko inayohusika.

Flaviana Mwimbe kutoka Zanzibar akizungumzia waajiri wa sekta ya utalii visiwani humo, alisema walilazimishwa kufunga hoteli na huduma na serikali chini bila kujali wamejiandaa au athari watakazozipata.

Alisema, hatua hiyo iliwaathiri waajiri na kuumiza wafanyakazi na kama kungekuwa na kipengele kwenye sheria cha kukabiliana na majanga ya maradhi, ungekuwa muongozo wakati wa corona.

Mkuu wa Programu na Sera utoka ActionAid, Jovina, akizungumza kwenye jukwaa hilo, alisema utafiti uliofanyika pamoja na maelezo ya serikali vinabainisha kuwa, kuna ongezeko la kazi nchini, lakini kazi hizo ni za staha?

Alisema, pamoja na changamoto za ukosefu wa ajira, vijana wengi wamekuwa na matatizo ya kutumikishwa, katika ajira zisizo na heshima ikiwamo kukosa mikataba, malipo duni, kutumikishwa muda mrefu bila kulipwa, kufukuzwa kinyume cha sheria na kwamba jukwaa hilo linalenga kushirikiana na wadau kupata ufumbuzi endelevu.

# Serikali yalinda wazalishaji wa vifaa vya umeme

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nishati, Medard Kalemani, ametangaza serikali kuzuia uingizaji holela wa viunganishi vya umeme kutoka nje ya nchi ili kuchochea uwekezaji katika kuzalisha vifaa vya umeme nchini.

Aidha, hatua hiyo ni ya kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Rais John Magufuli.

Akizungumza baada ya kuzindua kiwanda cha Polymeric Insulator cha jijini Dar es Salaam ambacho kinatengeneza vifaa vya kuunganisha mifumo ya umeme, Waziri Kalemani alisema kuwa mbali ya zuio hilo, serikali itawahakikishia wawekezaji hao soko la ndani la vifaa vyao vya umeme.

"Tangu mwaka 2017 tumewema mazuio kadhaa katika kuhakikisha vifaa vya umeme vinazalishwa hapa nchini ili kuunga mkono juhudi za serikali za ujenzi wa viwanda. Pamoja na mazuio hayo, leo (jana) natangaza kuzuia uingizwaji holela wa vifaa vya kuunganisha mifumo ya umeme (insulators) kwa lengo la kuchochea uwekezaji katika eneo hilo," alisema.

Alikisifu kiwanda hicho kwa kuzalisha vifaa hivyo na kusema lazima kuungwe mkono kwani hatua hiyo inaongeza upatikanaji wa ajira kwa vijana na kukuza pato la Taifa.

Aidha, ametaka Shirika la Umeme (TANESCO), Wakala wa Usambazaji wa Umeme Vijijini (REA) kushirikiana na Shirika la Viwango (TBS) kuhakikisha viwanda vinazalisha vifaa vyenye ubora na uwezo wa kushindana katika soko huria na kuwalinda watumiaji.

"Pamoja na kuhimiza uwekezaji katika viwanda, vyombo husika kama Tanesco, TBS na REA lazima vihakikishe bidhaa bora zinazalishwa ili kuwalinda watumiaji wa bidhaa zinazozalishwa ndani," alisema.

Mshauri Maalum wa viwanda cha Polymeric and Inhemeter, Dk. Adelhelm Meru, alisisitiza umuhimu wa taasisi nchini kutumia bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani kwani kwa kufanya hivyo zitakuwa zinachangia kudumisha ajira na kusaidia ukuaji wa uchumi.

"Hivi karibuni Tanzania iliingia uchumi wa kati, hivyo ni muhimu kuhimiza uzalishaji viwandani ili kuendelea kujenga uchumi imara na kukuza ajira," alisema Dk. Meru.

Dk. Meru aliyataka mashirika ya umma kuacha kuagiza vifaa vya umeme kutoka nje. Na kushauri kampuni ya nje kuwekeza nchini kwa kuwa mazingira ya uwekezaji yamerahisishwa sana.

"Serikali imefanya juhudi kubwa katika kuhakikisha panakuwapo na mazingira rafiki ya uwekezaji, hivyo nashauri mashirika ya umma yahimize wawekezaji kuja kuwekeza nchini badala ya kuagiza bidhaa hizo kutoka nje ya nchi," amesema katibu mkuu mstaafu wa wizara mbali mbali.

Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda hicho, Abraham Rajakili, aliishukuru serikali kwa kuwaunga mkono na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji, hatua hiyo imewarahisishia kwa kiwango kikubwa kufikia malengo yao.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU VITUO VYA UTANGAZAJI NCHINI VINAVYOJIUNGA NA VITUO VINGINE VYA UTANGAZAJI VYA NDANI NA NJE YA NCHI**

**1.0 UTANGULIZI**

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ina dhamana ya kusimamia Sekta ya Utangazaji pamoja na Sekta nyingine za Mawasiliano, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa vituo vya Utangazaji vinazingatia weledi wa vipindi na habari au matukio yanayorushwa na vituo vyao. Ili kuhakikisha kuwa vituo vya Utangazaji vinatimiza wajibu wao, TCRA hutumia Kanuni zinazosimamia Sekta pamoja na kutoa leseni zilizo na msharti (Licence conditions) ya jinsi ya kutoa huduma za Utangazaji nchini.

Kanuni ya 37 ya **"THE ELECTRONIC AND POSTAL COMMUNICATIONS (RADIO AND TELEVISION BROADCASTING CONTENT) REGULATIONS, za 2018"** ziliruhusu vituo vya Utangazaji kujiunga na kituo chochote cha utangazaji kwa ajili ya matangazo mubashara ili mradi kunakuwa na makubaliano ya kibiashara.

**2.0 UZOEFU ULIOPATIKANA**

Katika kusimamia utekelezaji wa Kanuni hii, kumekuwa na changamoto ya vipindi au habari zinazorushwa na vituo vya Utangazaji hasa ***pale vinapojiunga na vituo vya Utangazaji vilivyoko nje ya nchi na kurusha habari au matukio yanayohusu nchi yetu. Kwa mfano inapotokea dhahiri kuwa habari zinazohusu Nchi yetu hazikuzingatia maadili na weledi wa uandishi wa habari, huku habari hizo zikirushwa na vituo vilivyopewa leseni na TCRA, ni dhahiri hiyo inasababisha changamoto katika utekelezaji wa Kanuni hizo.***

**3.0 UTATUZI**

Ili kuweza kusimamia vizuri maudhui ya nje yanayorushwa mubashara, Kanuni ya 37 ilifanyiwa marekebisho mwaka 2020 kwa kuongeza kanuni ndogo (2) inayokitaka Kituo chochote cha Utangazaji kinachotaka kujiunga na kituo kingine cha ndani au nje ya nchi kwa ajili ya kurusha matangazo yake yakiwemo yale ya mubashara kupata kibali/ruhusa ya kufanya hivyo kutoka TCRA. Huu ni utaratibu tu wa kawaida na biashara zitaendelea.

Aidha, ifahamike kuwa marekebisho haya yanavihusu vituo vyote vya utangazaji vya Redio na Televisheni na watoa huduma za Maudhui Mtandaoni (Online Radio & Televisheni).

Hivyo TCRA inavielekeza vituo vya Utangazaji vinavyohitaji kurusha matangazo ya vituo vya Utangazaji vilivyoko nje ya nchi kuwasilisha makubaliano yao TCRA na kupata kibali kama utaratibu wa kawaida wenye lengo la kuleta ufanisi katika usimamizi wa maudhui yanayorushwa na vituo hivyo.

Kwa vituo ambavyo tayari wanarusha matangazo ya vituo hivi, vinatakiwa kuomba kibali/ruhusa husika na kuwasilisha makubaliano yao TCRA na sio kusimamisha matangazo au makubaliano yaliyopo. Huu ni utaratibu mzuri utakaoiwezesha TCRA kufahamu makubaliano hayo na kusimamia Sekta kwa ufanisi kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo.

Kwa hiyo, TCRA inavielekeza vituo vyote kuwasilisha maombi yao ndani ya siku saba (7) tokea kutolewa kwa taarifa hii.

**Ifahamike pia kwamba hoja kuu hapa ni vyombo vya Habari na si Waandishi wa Habari.**

**Imetolewa na:**

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania,**
**Mawasiliano Towers,**
**Kitalu Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma,**
**S. L. P 474,**
**14414 DAR ES SALAAM**

2158543O2

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Vyama vya siasa sasa viweke wazi ilani zao

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) inakamilisha utoaji wa fomu kwa wagombea urais na makamu wa rais wa Jamhuri ya Muungano, mchakato ambao unatarajia kufuatiwa na uteuzi.

Kukamilika kwa uteuzi kutatoa fursa kwa wagombea hao pamoja na wagombea wa ubunge na udiwani kuanza kampeni kwa pamoja Agosti 26, mwaka huu.

Watanzania wenye sifa ya kupiga kura katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu, wanachokisubiria ni kuanza kwa kampeni na kuwasikiliza wagombea na vyama vyao wanawaeleza nini katika suala zima la maendeleo.

Kwa maneno mengine, wanavisikilizia vyama vya siasa viweke wazi ilani zao za uchaguzi ili kuelewa ni mambo gani ya maendeleo vinatarajia kuwaletea wananchi na kupitia njia zipi ikiwa vitapata ridhaa ya kushika dola.

Kama ni afya, maji, miundombinu, elimu, basi kinapaswa kueleza ni kwa namna gani, lakini pia kueleza ni kwa jinsi gani fedha za kutekeleza miradi hiyo zitapatikana.

Ilani ya uchaguzi ni nguzo muhimu katika uchaguzi mkuu, kama kuna chama hakijaandaa ilani kisha kikasimama kwa wananchi kuomba kura basi chama hicho kijue kuwa hakijawatendea haki, na hakistahili kupewa kura.

Tumeamua kuzungumzia suala la umuhimu wa vyama vya siasa kuandaa ilani na kuziweka wazi kwa ajili ya uchaguzi mkuu kwa kuwa inaonekana halipewi kipaumbele na baadhi ya vyama.

Ni kweli kwamba ilani ya uchaguzi hutumiwa na vyama na wagombea wao kwenye majukwaa ya kampeni kujinadi kwa wananchi, lakini hadi sasa kuna vyama ambavyo havionekani kama vimeandaa ilani kwa ajili ya uchaguzi wa Oktoba.

Kilichotushangaza na kinachoendelea kutushangaza ni kuwa baadhi ya wagombea urais hawajazungumzia chochote kuhusu ilani za vyama vyao. Tulichoshuhudia ni kusikia kauli zao kwenye mikutano ya kuteuliwa na vyama vyao na wakati wa kuchukua fomu NEC.

Tena wengine wanatoa kauli za mzaha, wakati kugombea nafasi ya urais ni jambo kubwa na zito, ambalo linapaswa kuchukuliwa kwa uzito na umakini mkubwa.

Ingawa suala la vyama vya siasa kuwa na ilani sio takwa la kisheria, lakini kwa mazingira ya nchi ambazo hazijawa na ukomavu katika demokrasia ya ushindani wa vyama, linaweza kuleta shida inapoweza kutokea chama fulani kikashinda uchaguzi bila kuwa na ilani.

Tunasema hivyo kwa kuwa kinaweza kushindwa kuwajibika kutokana na kutotoa ahadi kimaandishi kuhusiana na mambo kitakayowafanyia wananchi.

Ziko faida nyingi kwa vyama kuwa na ilani, zikiwamo vyama kuwajibika kwa wananchi kwa kuahidi mambo ambayo vinakusudia kuyafanya na kuvifanya kuzungumzia ajenda za msingi katika majukwaa ya kampeni badala ya kuzungumzia mambo ambayo hayawezi kutekelezeka.

Chama ambacho hakina ilani ya uchaguzi kinakwenda kwenye majukwaa ya kampeni kuzungumza mambo ya hovyo, matusi na wakati mwingine kuwashambulia wagombea pamoja na vyama vingine.

Kwa kuwa sheria ya uchaguzi nchini haivibani vyama vya siasa kuwa na ilani za uchaguzi, tunafikiri kwamba jambo hili linapaswa kuangaliwa upya ili kuliweka liwe takwa la kisheria kwa nia njema.

Tunavishauri vyama vyote ambavyo vinashiriki katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu kuweka hadharani ilani zao ili wapigakura wajiue kabla ya kuamua ni chama na wagombea wapi wawapigie kura ifikapo siku ya uchaguzi.

Tunasisitiza kuwa haileti picha nzuri kwa baadhi ya vyama kutokuwa na ilani za uchaguzi badala yake vyama vichache kuwa nazo. Hatuamini kuwa gharama ndizo zinazovikwamisha kwa kuwa vinaweza kuziandaa kwa gharama ndogo za ushauri wa wataalamu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kampeni, ushawishi uwe sera si mlungula

OKTOBA 28, mwaka huu, Watanzania watapiga kura kuwachagua rais, wabunge na madiwani ikiwa ni baada ya zaidi ya miezi miwili ya kampeni za uchaguzi huo utakaoshirikisha wagombea wa vyama mbalimbali vya siasa.

Ratiba ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), inaonyesha kuwa kampeni za uchaguzi huo zinatarajia kuanza rasmi Agosti 26 hadi Oktoba 27 na kufuatiwa uchaguzi wenyewe siku inayofuata.

Katika kipindi hicho cha zaidi ya miezi miwili, wagombea wa nafasi ya urais, ubunge na udiwani waliopitishwa na vyama vyao, watanadi sera na ilani za vyama vyao kwa wapigakura ili wawachague.

Uchaguzi wa mwaka huu utakuwa na mabadiliko kidogo ya siku, kutoka Jumapili hadi katikati ya wiki, ambayo itakuwa siku ya Jumatano, na sasa kuna hatua mbalimbali zinaendelea kufanyika ili kufanikisha uchaguzi huo.

Miongoni mwa hatua hizo ni wagombea kuchukua fomu za kuwania urais, ubunge na udiwani, huku vyama vingine vikiwa, katika mchujo wa kupata wanachama wa kuviwakilisha katika uchaguzi huo.

Wakati hatua mbalimbali zikiendelea kwa ajili ya kufanikisha uchaguzi huo, vyema pia kuwakumbusha Watanzania kuwa makini, kwamba, wajikite katika maandalizi ya kupiga kura, ili kupata viongozi bora na siyo bora viongozi. Hatua hiyo itawasaidia kuepuka kuchagua wagombea ambao hawana manufaa kwa maendeleo ya maeneo yao, hivyo wasichukulie wakati huu kama wa kula na kujikuta wakichagua wagombea wasiofaa.

Ikumbukwe kwamba, katika kampeni za uchaguzi, wagombea hutumia mbinu nyingi, kwa lengo la kuwaweka sawa wapigakura, hali ambayo inaweza kusababisha 'wanakula badala ya kupiga kura'.

Siyo jambo la kushangaza kuta wagombea wakiingia nyumba kwa nyumba mara baada ya kampeni, wakati wa usiku kwa lengo la kurubuni wapigakura kwa kuwapa chochote ili wawachague. Mtindo huo ni sawa na kula siyo kura.

Huu sasa ni wakati wa kura siyo kula, wananchi wakiendeleza kula watajikuta wanachagua watu wasiofaa, hivyo watumie haki yao ya kikatiba ya kuchagua viongozi wanaotaka, lakini si kwa kigezo cha kupewa chochote.

Watanzania wanahimizwa kujiandikisha, katika daftari la kudumu la wapigakura, lengo ni kutaka wawe na haki ya kushiriki kwenye uchaguzi huo, hivyo wasikubali kuipoteza kwa kuchagua wagombea wasiofaa.

Julai, mwaka jana wakati akizundua rasmi uboreshaji wa daftari hilo, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alihimiza vijana waliotimiza miaka 18 kujitokeza kwa wingi kujiandikisha kwa kuwa bila kujiandikisha hawawezi kushiriki uchaguzi.

Kwa mantiki hiyo walioajiandikisha katika daftari hilo, watumie haki hiyo kuchagua viongozi sahihi watakaowaletea maendeleo na kuachana na wale wenye mpango wa kutoa chochote ili wachaguliwe.

Wanasiasa nao wawaache wapigakura, waamue wenyewe kuchagua viongozi wanaowataka, bila kuwapo kwa mbinu zozote chafu zinazoweza kuwaingiza katika mtego wa kuchagua kula badala ya kura.

Kila upande ukitimiza wajibu, hakutakuwa na wagombea wa kuingia nyumba kwa nyumba wakati wa usiku, kwa lengo la kurubuni wananchi kwa chochote ili wawapigie kura, watakuwa huru kuchagua viongozi wanaowataka.

Ikumbukwe kuwa uzoefu unaonyesha kuwa kuna mchezo huo ambao wakati mwingine baadhi ya wagombea hudaiwa kuwapa wapigakura vitu ili wawachague.

Wanavyopewa ni pamoja na khanga, kofia, fulana na hata wakati mwingine fedha, ikiwa ni mojawapo na ushawishi kwa wananchi, ili watoe kura zao kirahisi kwa wagombea wasiofaa.

Yawezekana kukawa na mtifuano mkali kutoka kwa wagombea watakaopitishwa na vyama vyao, hivyo ni muhimu wananchi kuwa makini, ni la msingi kwa kuwa huenda baadhi wakatumia mbinu chafu kupata ushindi.

"Wapo wanasiasa kutoka vyama mbalimbali wenye ushawishi mkubwa kwa wananchi, kinachotakiwa ni ushawishi wa sera na ilani za vyama uwe msingi wa kuwapigia kura, si mbinu za kutoa chochote.

Mgombea mwenye lengo la kuleta maendeleo hapaswi kutumia ujanja ujanja kutafuta uongozi, badala yake anaweka wazi kile anachotaka kuwafanyia wananchi ili waamue.

HABARI KITAIFA

# Wadau wa uhifadhi wasaidia kudhibiti uharibifu wa tembo

**Na Beatrice Shayo, RUFUJI**

WADAU wa masuala ya hifadhi wamesaidia kupunguza migogoro ya tembo na wakulima katika kijiji cha Ngarambe Wilaya ya Rufuji mkoani Pwani baada ya kuanza kutumia mbinu mpya ya pilipili katika mashamba yao.

Hayo yalibainishwa na Mhifadhi wa Wanyamapori Wilaya ya Rufiji, Mwarabu Mpunde, alipokuwa akizungumza na wanahabari wakati wa ziara iliyofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID).

Mpunde alisema mbinu mpya ya elimu ya fensi ya pilipili imesaidia katika kupambana na tembo ili wasiendele kula mazao yao.

Alisema unachukua pilipili na oil chafu unafunga kwenye kitambaa na kupaka mafuta hayo kwenye kitambaa kisha kuzungusha katika eneo la shamba.

"Mbinu hiyo imesaidia kwa sababu tembo anavyokuja katika eneo la shamba akisikia harufu ya pilipili inamfanya apige chafya, hivyo pilipili hizo zinakuwa kama zinamchoma anapopumua na kuamua kuondoka," alisema Mpunde.

Mpunde alisema yeye ni miongoni mwa watu waliopewa mafunzo kuhusiana na mbinu hiyo na tayari wameifanyia kazi hiyo katika baadhi ya maeneo na imeleta tija.

Alisema kijiji cha Ngarambe wamevuna tani 20 za mahindi kwa kipindi cha mwaka huu, jambo ambalo sio la kawaida.

"Kama tumesikia kuna taarifa ya tembo tunatumia vipuri ila kuna tembo wengine wakiwa eneo la hifadhi ni ngumu kuondoka kwa vile ile milio wameshaizoea wakiwa ndani ya hifadhi hasa katika eneo la Ngarambe na Mloka," alisema.

Aidha, alisema bado changamoto ipo kwenye kijiji cha Ngolongo hadi Mloka kwani tembo wamekuwa wakiwatesa wananchi na hawajapatiwa elimu ya kutumia pilipili.

"Kipindi cha kilimo hasa kwenye msimu wa embe ama korosho huwezi kumfukuza tembo... hii nayo ni changamoto, inafika wakati hata kama embe zimebaki chache atazunguka na kurudi tena," alisema.

Alisema wakulima wanapovuna mazao yao na kuyahifadhi kwenye ghala tembo hubomoa na kuyala.

Alisema zaidi ya watu 100 wamepatiwa taarifa ya mazao yao kuliwa na tembo, na tayari majina yao wameyawasilisha ngazi husika ili waweze kupatiwa fidia ya kifuta macho.

Aidha, Mpunde alisema idara ya wanyamapori ina changamoto kubwa ya vifaa vya kufanya kazi, likiwamo gari.

Alisema wanaweza kupata taarifa kutoka Kijiji cha Mloka mpaka wawafikie wananchi inapita wiki moja, hivyo wanajikuta hawafiki kwa wakati.

Alisema idara yao walikuwa na gari ambalo waliazima kutoka idara nyingine, lakini limechukuliwa wamebaki bila gari.




Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa Benki ya NMB, Alex Mgeni, akizungumza kwenye kongamano la biashara lililoandaliwa na benki hiyo mjini Geita, ili kuwafunda wafanyabiashara 150, kuhusu huduma za kifedha na faida za kutumia benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAKUKURU yaahidi kupambana na ujangili

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imesema imejipanga kuhakikisha rasilimali za misitu hapa nchini zinalindwa na yeyote atakayekutwa atahesabika kama ni jangili na hatua kali dhidi yake zitachukuliwa.

Kauli hiyo ilitolewa na Ofisa wa TAKUKURU kutoka makao makuu, Ally Katonya, akitoa mada kwenye mafunzo waandishi wa habari wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (JET), yaliyofanyika kwa njia ya Mtandao chini ya Ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID).

Katonya alisema misitu pamoja na maliasili ikiwamo wanyama ni moja ya rasilimali muhimu kwa taifa kwa kuwa zinachangia kuleta nishati, maji na kuhifadhi mazingira huku wanyama wakililetea taifa fedha za kigeni ambazo zinachangia kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema kwa kushirikiana na taasisi nyingine za serikali ikiwamo Wizara ya Maliasili, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka makao makuu, wameweka nguvu ya pamoja na kwamba yeyote atakayekutwa kwenye mapori ya wanyama na hifadhi za misitu akifanya uhalibifu atahesabika kama ni jangili na mali zake zitataifishwa ikiwamo kufunguliwa kesi za uhujumu uchumi.

"Tukikubaini umeua tembo au mnyama yeyote yule na ukauza na kununua gari au nyumba, kwanza tutataifisha hizo mali zako na pia tutakufungulia kesi ya uhujumu uchumi kwa kuwa umeuhujumu rasilimali za taifa letu," alisema Katonya.

Kwa upande wake, Victoria Michael, kutoka Taasisi ya Sekta binafsi nchini (TPSF), akiwasilisha mada kuhusu mapambano dhidi ya vita ya ujangili, alisema si ya serikali pekee bali ni sekta binafsi ya kutambua hilo tayari wameshaanza kutoa elimu kwa wadau hao.

Alisema kuwa TPSF imeshaanza kuelimisha wadau wake na kwa kuwashirikisha katika miradi mbalimbali ya kuhifadhi rasilimali za misitu ili nao watoe mchango mkubwa kwa taifa ikiwamo mapambano ya kuzuia utorashaji wa wanyama, ujangili pamoja uhifadhi wa mazingira.

Alisema tayari wameanzisha kamati ambayo itasaidia kutatua changamoto zinazoikabili sekta ya uhifadhi wa mazingira na wanyamapori ili kusaidia serikali dhidi ya mapambano hayo.

Mkurugenzi wa JET, John Chikomo, alisema mafunzo hayo ni kuhakikisha wanapata uelewa wa masuala ya wanyamapori na uhifadhi ikiwamo sekta binafsi kutumia fursa ya kuwekeza katika sekta hiyo.

## NIT kuisaidia TAZARA, wahandisi wa mitambo

**Na Gwamaka Alipipi**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), kinatarajia kulisaidia Shirika la Reli la Tanzania na Zambia (TAZARA), kwa kuwapatia wahitimu wa fani ya uhandisi wa mitambo, ili shirika hilo liweze kuinuka na kujiendesha kwa ufanisi zaidi.

Mkuu wa chuo hicho, Prof. Zacharia Mganilwa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa ziara ya wajumbe wa Baraza la Uongozi wa NIT, walipotembelea shirika hilo, kwa lengo la kuongeza ushirikiano.

"Tuna vijana wengi waliohitimu uhandisi na hawana kazi, TAZARA wangetoa nafasi za kazi za kujitolea kwa vijana waliohitimu masuala ya uhandisi wa mitambo, nina imani shirika litainuka na kuwa bora zaidi, lakini tutaangalia namna ya kutoa msaada kwao," alisema Prof. Mganilwa.

Kadhalika, alieleza kuwa, vijana hao wakipewa fursa ya kujitolea kufanya kazi katika shirika hilo, watasaidia kwa asilimia kubwa kulifikisha katika hatua ya juu ya kiutendaji, kwa sababu kwa sasa wanakabiliwa na changamoto nyingi ukiwamo uhaba wa wafanyakazi.

Prof. Mganilwa alisema NIT inatoa mafunzo ya aina mbalimbali ya uhandisi, hivyo inaweza kuwaleta wanafunzi hao TAZARA kuja kufanya mafunzo kwa vitendo na kuongeza ujuzi wao.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya NIT, Prof. Bavo Nyichomba, alisema wamelazimika kufanya ziara TAZARA ili kuongeza maeneo ya ushirikiano.

"Tumekuja kuangalia maeneo ya kutoa ujuzi, TAZARA inahitaji wahandisi na sisi tunatoa mafunzo ya uhandisi hivyo tunaweza kushirikiana katika nyanja hiyo, Ni suala la kufahamu wao wanahitaji nini na sisi tunatoa nini" alisema Prof. Nyichomba.

Kaimu Mkurugenzi Msadizi wa TAZARA, Geoffrey Sengo, alisema wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo uhaba wa wafanyakazi, mtaji, kupokea mizigo michache kulikosabishwa na mlipuko wa ugonjwa wa corona. "Idadi ya wafanyakazi waliojariwa ni 2,775, mwaka jana walistaafu 400, na kwa sasa waajiriwa wengi wapo katika umri wa kustaafu, hivyo nguvu kazi inazidi kupungua," alisema Sengo.

Aliongeza kuwa idadi ya mizigo ambayo inasafirishwa na TAZARA kwa mwaka ni tani milioni tatu, kati ya idadi hiyo tani 200,000 za madini ya Graphite ni kutoka Tanzania na tani 600,000 za madini ya Lithium ni kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

# NBC yachangia mil. 111/- kuboresha elimu, kilimo

**Na Mwandishi Wetu, BARIADI**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imetoa Sh. milioni 114.7 kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya kilimo na elimu mkoani Simiyu ikiwa ni sehemu ya mkakati wa benki hiyo kuunga mkono jitihada za serikali katika kuendeleza sekta hizo.

Akipokea mchango huo kwenye hafla maalum iliyofanyika kwenye Maonyesho ya Kilimo (Nanenane) kitaifa, mkoani Simiyu, Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, alisema sehemu ya fedha hiyo itumike kujenga kisima cha Shule ya Sekondari ya Wasichana Maswa na kuandaa shamba la hekari 50 litakalokuwa na alama ya benki hiyo.

"Kwa kuwa benki ya NBC imekuwa mstari wa mbele katika kutusaidia hasa katika masuala yanayoacha alama kama haya ya ujenzi wa miundombinu ya elimu na sekta ya kilimo na sisi kama mkoa tumeona ipo haja ya kutambua mchango huo kwa kuwapatia heshima hiyo wanayostahili," alisema

Aliipongeza benki hiyo kwa kuteuliwa kuwania tuzo uzo za ubora za Afrika katika kuwahudumia wajasiriamali ambazo zinaakisi ufanisi wa benki hiyo katika kutoa huduma za kibenki na kifedha katika bara la Afrika.

"Ni heshima kubwa kwa benki ya NBC na taifa kwa ujumla kuingia kwenye orodha ya benki tano bora zinazowania tuzo ya Benki Bora ya mwaka ya Wajasiriamali (SME miongoni mwa benki zaidi ya 200, hatua muhimu zaidi kufikiwa na benki ya Kitanzania ndani ya mwaka huu." Alibainisha.

Akitoa mchanganuo wa fedha hizo Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, alisema kiasi cha Sh. milioni 40 ni udhamini wa benki hiyo kwenye maonyesho hayo, huku kiasi cha Sh. milioni 10 kikilenga kuchangia ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Simiyu ambapo kitatosha kugharamia mifuko ya 541 ya saruji.

"Aidha kiasi cha milioni 19.9 kitakwenda katika kusaidia ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Anthony Mtaka ambapo kiasi hicho kitatosha kununua mifuko ya saruji 1,080 na kiasi cha Sh. milioni 44.8 kitatumika kugharamia uchimbaji wa kisima cha umwagiliaji wa mashamba ya viazi kwa vikundi vya akina mama wilayani Maswa," alisema.

Sabi alitaja baadhi ya jitihada za benki hiyo katika kuwahudumia wajasiriamali na wakulima kuwa ni pamoja na uendeshaji wa mafunzo maalumu ya kilimo na biashara kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wafanyabiashara wanawake na Vijana (TABWA) pamoja na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) yanayofanyika kwenye maonyesho hayo.

# Mtendaji atuhumiwa kuuza ardhi, arudisha nusu ya fedha

**Na Frank Kaundula, MVOMERO**

MKUU wa Wilaya ya Mvomero, Alibinus Mgonya, amemuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya hiyo kumchukulia hatua za kinidhamu Mtendaji wa Kijiji cha Madaraka, Lamerk Kajiru, anayetuhumiwa kuuza ardhi kwa Sh. milioni tano.

Alitoa agizo hilo jana, baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi wa kijiji hicho, Kata ya Doma kwenye mkutano wa kijiji yanayomtuhumu Mtendaji huyo kuuza ardhi yenye ukubwa wa ekari 100.

"Namuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri kumchukulia hatua za kinidhamu mtendaji huyo anayedaiwa kuuza ardhi yenye ukubwa wa ekari 100 kwa Sh. milioni tano bila kufuata utaratibu wa serikali unaotakiwa," alisema Mgonya.

Mgonya alisema, Mtendaji huyo anadaiwa kuuza ardhi hiyo na kisha fedha kuzitumia kwa matumizi yake binafsi jambo ambalo kamwe haliwezi kukubalika katika wilaya hiyo kwa kuwa ni moja vitu vinavyochochea migogoro ya ardhi.

Alisema serikali imejitahidi kudhibiti migogoro ya ardhi katika wilaya hiyo, lakini kuna baadhi ya watu ambao ni watumishi wa umma wanatumia madaraka yao vibaya na kusababisha kuchochea migogoro nchini.

Alisema akiwa Mwenyetiki wa ulinzi na usalama katika wilaya hiyo, hawezi kuona mtu au watu wakiendelea kufanya kazi ya kuwahujumu wananchi hususani wanyonge na lazima sheria ifuate mkondo wake ili iwe fundisho.

"Serikali ya awamu ya tano imekuwa ikiwasisitiza watendaji kushughulikia changamoto mbalimbali za wananchi ili kuzitatua na kuondoa migogoro yote kwenye jamii hivyo suala hili halipaswi kufumbiwa macho," alisema Mgonya.

Aliwataka wananchi wa kijiji hicho kuwa watulivu wakati suala la tuhuma za mtendaji huyo zikishughulikiwa na kuwasihi kuendelea na majukumu yao ya uzalishaji wa mali kwa maslahi ya taifa. Aliwataka wananchi wa kijiji hicho kujiandaa na msimu mpya wa kilimo ili mvua zitakapoanza kunyesha waweze kulima mazao mengi ya chakula na biashara ili wilaya ipate mapato mengi ya ndani yatokanayo na ushuru.

Mtendaji anayetuhumiwa, Lamerk Kajiri, alikiri kufanya kitendo hicho na kuomba radhi kwa mkuu wa wilaya na kuamua kurejesha Sh. 2,500,000 na kuahidi kurejesha kiasi kilochibaki kabla ya Novemba 4, mwaka huu.

Wananchi wa kijiji hicho walimshukuru Mkuu wa wilaya hiyo kwa kitendo cha kulishughulikia haraka suala hilo na kuahidi kuendelea kutoa ushirikiano kwa serikali na kuwafichua watumishi wasiokuwa waadilifu kazini.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mbezi Ndumbwi, iliyopo Mbezi Makonde jijini Dar es Salaam, wakinawa mikono baada ya kutoka kwenye mtihani ikiwa ni sehemu ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa Covid-19. **PICHA: GIDION MSABULA/TUDARCO**

# Wazee 200 wapata matibabu ya bure

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

ZAIDI ya wazee 200 katika Kata ya Mkuza, Halmashauri ya Mji wa Kibaha, wamepatiwa huduma ya matibabu bure kutoka Shirika la Tunajali.

Akizungumza na Nipashe juzi katika eneo la Kwa Matiasi, Mkurugenzi wa Shirika hilo, Nicas Mawazo, alisema wanalenga kuwafikia wazee wengi zaidi katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

Nicas alisema shirika hilo limekuwa likitoa huduma kwa watu wote kwa gharama nafuu na sasa wameamua kutenga siku maalumu kwa kila mwezi kutoa matibabu ya kibingwa kwa magonjwa ya kisukari na moyo na kwamba wazee watafanyiwa uchunguzi wa kina.

"Jamii inatakiwa kutamani kusaidia wengine kwa kile walicho nacho. Sisi kwa upande wetu tutaendelea kutoa huduma hii. Tumeanza na kata baadaye tutafikia kata zote za halmashauri hadi ngazi ya mkoa tuguse makundi maalumu na kuibua shida zao ambazo zitapatiwa ufumbuzi," alisema.

Mmoja wa wazee walionufaika na huduma hiyo, Mohamed Mgoha, alilishukuru shirika hilo kwa kuwasogezea huduma karibu na maeneo yao kwa kuwa si wote wenye uwezo wa kufika kwenye vituo vya huduma za afya.

Naye Gerson Kauga alilishukuru shirika hilo kwa kuwakumbuka wazee na kuomba wahisani wengine kuiga mfano na kuwajali wazee ambao wamekuwa wakipata changamoto katika huduma za afya.

Pily Yahaya, ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Kata ya Picha ya Ndege, aliiomba serikali kutoa ushirikiano kwa shirika hilo ili liwafikie wazee wengi zaidi.

**"Jamii inatakiwa kutamani kusaidia wengine kwa kile walicho nacho. Sisi kwa upande wetu tutaendelea kutoa huduma hii. Tumeanza na kata baadaye tutafikia kata zote za halmashauri hadi ngazi ya mkoa tuguse makundi maalumu na kuibua shida zao ambazo zitapatiwa ufumbuzi," alisema.**

HABARI KITAIFA

# Ataka uwazi usomaji mita

Na Neema Hussein, KATAVI

NAIBU Waziri wa Maji, Juma Aweso, amezitaka Mamlaka za Maji nchini kuwashirikisha wananchi wanaotumia maji pale wanapokwenda kusoma bili za maji ili kuepuka malalamiko ya kuzidishiwa bili hiyo.

Aweso aliyasema hayo juzi katika ziara ya kukagua miradi mbalimbali ya maji mkoani Katavi likiwamo tangi la maji linalojengwa katika Mtaa wa Mapinduzi, Manispaa ya Mpanda ambalo litakamilika Septemba 15, mwaka huu.

Ikitokea mwananchi amekatiwa maji akiwa tayari amelipia bili, alisema inatakiwa arudishiwe maji hayo ndani ya saa 24 na mtu anapotaka kuunganishiwa maji na amelipia bili za kuunganishiwa, inatakiwa ndani ya siku saba mtu huyo apate maji.

"Naomba muwafikishie EWURA (Mamlaka ya Huduma za Nishati na Maji), wambieni wajitafakari juu ya bili za maji, lazima watoke ofisini wasimamie bei za maji kwa wananchi hawa wanyonge kuhakikisha wanalipa bili zilizo sahihi," alisema Aweso.

Alisema wameleta zaidi ya Sh. bilioni 5.6 katika Mkoa wa Katavi kwa ajili ya kumaliza tatizo la maji vijijini na tayari kuna miradi 19 inayotekelezwa katika halmashauri zote 5 kwa Mkoa wa Katavi huku akibainisha kuwa katika Wilaya ya Tanganyika, walitoa bilioni 1.3.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda, Mhandisi Iddo Richard, alisema mradi wa maji wa Ikolongo ukikamilika utapunguza mgawo wa maji na wananchi wa mpanda watapata maji kwa asilimia 60.

**Naomba muwafikishie EWURA (Mamlaka ya Huduma za Nishati na Maji), wambieni wajitafakari juu ya bili za maji, lazima watoke ofisini wasimamie bei za maji kwa wananchi hawa wanyonge kuhakikisha wanalipa bili zilizo sahihi.**

# Ashtakiwa kukusanya bil. 17/- bila leseni

Na Hellen Mwango

MFANYABIASHARA Tariq Machibya (29), maarufu kama Mr Kuku, amefikishwa mahakamani akikabiliwa na mashtaka saba likiwamo la kujihusisha na biashara ya upatu kwa kukubali na kukusanya Sh. bilioni 17 kutoka kwa umma bila leseni.

Mshtakiwa huyo ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Mr Kuku Farmer Ltd, alisomewa mashtaka yake katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi Godfrey Isaya.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa Januari 2018 mpaka Mei, mwaka huu katika mahali tofauti jijini Dar es Salaam, alijihusisha na biashara ya upatu kwa kukusanya fedha kutoka kwa umma.

Ilidaiwa kuwa, mshtakiwa alikusanya fedha hizo kwa madai ya kufanya ujasiriamali wa ufugaji wa kuku na wangepata faida ya asilimia 70 ya mtaji waliowekeza kwa miezi minne ya awali na asilimia 90 ya mtaji kwa miezi sita kiasi ambacho ni kikubwa kibiashara kuliko mtaji uliowekezwa.

**Baada ya kusomewa mashtaka hayo, Wakili Wankyo alidai, upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kesi iliahirishwa hadi Agosti 24, mwaka huu.**

Wakili Wankyo alidai kati ya Januari, 2018 na Mei, 2020, maeneo tofauti jijini Dar es Salaam, alikubali na kupokea Sh. bilioni 17 kutoka kwa umma bila kuwa na leseni.

Ilidaiwa kwamba, kati ya Aprili 26, 2019 na Januari, 2020 jijini Dar es Salaam, alijihusisha na muamala wa Sh. 6, 477,297,614.83 kwa kuzitoa kutoka kwa akaunti ya Mr Kuku iliyopo benki ya CRDB wakati akifahamu zimetokana na kosa la kujihusisha na biashara ya upatu.

Mshtakiwa huyo pia anadaiwa kwamba kati ya Januari na Machi 30, mwaka huu, jijini Dar es Salaam, alitakatisha Sh. 629,249,576.36 kwa kuzitoa kutoka akaunti ya CRDB wakati akijua zilitokana na kosa la upatu.

Wakili Wakyo alidai kati ya Machi 5 na Aprili 17, mwaka huu, alitakatisha Sh. 1,366,718,045.46 kwa kuzitoa kutoka akaunti ya Mr Kuku Farmers Ltd, iliyopo benki ya CRDB.

Aliongeza kuwa kati ya Januari 17 na 30, mwaka huu, jijini Dar es Salaam katika tawi la CRDB Viva Tawar, Kinondoni, Dar es Salaam, alitakatisha Dola 107,893.73 kwa kuzitoa na kuziingiza katika akaunti ya Mr Kuku wakati akijua zilitokana na biashara ya upatu.

Wankyo alidai kati ya Machi 3 hadi 30, mwaka 2020 benki ya CRDB Water Front, Machibya alijihusisha na muamala wa dola 146, 300 na kuziingiza katika akauti ya Mr Kuku Farmers Ltd wakati akijua fedha hizo zilitokana na upatu.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, Wakili Wankyo alidai, upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kesi iliahirishwa hadi Agosti 24, mwaka huu.

Mshtakiwa alipelekwa rumande kwa kuwa mashtaka ya utakatishaji hayana dhamana.



Mkuu wa Mauzo wa Vodacom Kanda ya Kaskazini, George Venanty (katikati), pamoja na wafanyakazi wenzake wakisherehekea baada ya kampuni hiyo kuibuka mshindi wa kwanza kwa kampuni za mawasiliano, wakati wa kilele cha maonyesho ya wakulima (Nanenane), katika viwanja vya Themi, jijini Arusha. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Waziri atangaza neema wakulima wa pamba

Na Mwandishi Wetu, SHINYANGA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, ameeleza kuridhishwa na ununuzi wa pamba msimu wa mwaka 2020/21 huku akitangaza mapinduzi makubwa katika kilimo.

Hasunga alisema hayo juzi huku akisisitiza kuwa serikali imedhamiria kuhakikisha wakulima wanaondoka katika dhana ya kilimo cha kujikimu badala yake kuwa kilimo cha kibiashara. Waziri alisema hayo alipokuwa ziarani katika mikoa ya Singida na Tabora.

Alisema ili kusimamia jambo hilo kwa vitendo, serikali imeanza kutoa elimu kwa wakulima kupitia maofisa ugani na wataalamu mbalimbali wa kilimo kuhusu namna bora ya kuzingatia mbinu bora za kilimo ili kuongeza tija na uzalishaji.

Katika ziara hiyo, Hasunga aliwahakikishia wakulima kuwa, serikali inasimamia kwa weledi mkubwa sekta ya kilimo ambayo ndiyo mhimili mkubwa wa maendeleo ya wananchi na inachangia kwa asilimia kubwa uchumi wa nchi.

Hasunga alisema ili kuboresha kilimo na maisha ya wakulima, ni dhahiri kuwa serikali lazima ifanye mazungumzo na benki mbalimbali ikiwamo Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) kwa ajili ya kupunguza riba na masharti magumu kwa wakulima ili wakope kwa ajili ya kuboresha kilimo.

Akiwa wilayani Iramba, mkoani Singida, Waziri Hasunga alipongeza kampuni ya ununuzi wa pamba ya Biosustain kwa kuhakikisha imemaliza madeni yote ya wakulima kwa msimu wa mwaka 2018/19.

Waziri alisema pamoja na changamoto iliyojitokeza ya ugonjwa wa mapafu (COVID-19) kampuni hiyo imehakikisha wakulima wote wanalipwa fedha zao kwa wakati.

# Wasimamizi uchaguzi waonywa ukada

Na Neema Hussein, RUVUMA

WASIMAMIZI wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata katika jimbo la Mbinga Mjini mkoani Ruvuma, wameonywa kujiepusha kufanyakazi kwa itikadi za vyama na kupendelea wagombea.

Badala yake wametakiwa kutenda haki kwa kila chama wakati wote wa mchakato wa uchaguzi ili kuepusha vurugu na malalamiko.

Ofisa Uchaguzi Jimbo la Mbinga, Amon Sangana, alisema hayo juzi wakati akifunga mafunzo ya siku tatu ya kuwajengea uwezo wasimamizi wasaidizi 38 wa uchaguzi ngazi ya kata na jimbo. Mafunzo hayo yanalenga kuwaongoza katika mchakato mzima wa maandalizi ya uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba, mwaka huu.

Sangana aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kwenda kutekeleza vyema yale waliyofundishwa ikiwamo uadilifu, weledi na kujiepusha na aina yoyote ya upendeleo kwa vyama vya siasa na wagombea.

**Katika mchakato wa uchaguzi ni lazima mgombea awe amedhaminiwa na chama cha siasa, amethibitishwa na hakimu au wakili pamoja na kutoa fedha ya dhamana.**

Sangana alisema katika mchakato wa uchaguzi ni lazima mgombea awe amedhaminiwa na chama cha siasa, amethibitishwa na hakimu au wakili pamoja na kutoa fedha ya dhamana.

Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Mbinga Mjini, Grace Quintine, alisema matumaini ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ni kwamba baada ya kupata mafunzo hayo watakwenda kufanya kazi kwa juhudi, maarifa na weledi wa hali ya juu.

Quitine ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Mbinga, alisema wakati wote wa mchakato wa uchaguzi mkuu, watafanya kazi kwa kufuata maelekezo ya tume na msimamizi wa uchaguzi ngazi ya jimbo na kushirikiana na vyama vyote vya siasa vitakavyoshiriki katika uchaguzi huo.

Aidha, alisisitiza kuzingatia maadili ya utumishi wa umma wakati wa mchakato wa uchaguzi pamoja na kufanya kazi zingine za utumishi ikiwamo kuuza vitambulisho vya wajasiriamali vilivyotolewa na Rais John Magufuli.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo, Asha Chowo na Benito Komba, walisema mafunzo hayo yamekuwa mazuri kwa sababu yamewapa uelewa katika usimamizi wa uchaguzi mkuu na uzoefu wa kwenda kutekeleza majukumu ya NEC.

Chowo aliishukuru Halmashauri ya Mji Mbinga kwa kuwajengea uwezo na uelewa katika majukumu yao ya usimamizi wa uchaguzi mkuu.

Alisema kimsingi mafunzo hayo yamewapa dira namna ya kwenda kutekeleza majukumu yao ikiwamo kushirikiana na vyama vya siasa, wananchi na mchakato na namna ya kutumia kanuni na taratibu zilizoainishwa na tume.




Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga (kushoto), akikabidhi tuzo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, ukiwa ni utambuzi wa benki hiyo kama mdhamini mkuu wa Maonesho ya Kilimo ya Nanenane yaliyomalizika mkoani Simiyu. **NA MPIGAPICHA WETU**

# RC ataka matofali bei nafuu ujenzi madarasa

Na Alphonce Kabilondo, GEITA

SERIKALI mkoani Geita imewaagiza wakuu wa wilaya, wakurugenzi watendaji wa halmashauri na maofisa elimu kutumia matofali fungamano ili kupunguza gharama za ujenzi wa vyumba vya madarasa katika maeneo yaliyo na upungufu wa madarasa.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel, alitoa agizo hilo juzi katika Shule ya Msingi Nyanza, Halmashauri ya Mji wa Geita, wakati akipokea taulo 215 za wanafunzi wa kike wanaosoma shule za msingi na sekondari zilizotolewa na shirika la Plan International kwa ajili ya kujihifadhi wakati wa hedhi wawapo shuleni.

Alisema serikali ya mkoa ilijiwekea lengo la kufyatua matofali fungamano 16,7100,673 ili kumaliza upungufu wa madarasa kwa maeneo yaliyo na changamoto hiyo lakini mpaka sasa matofali 400,000 tu ndiyo yamefyatuliwa.

Matofali hayo, alisema yatapunguza gharama za ujenzi wa madarasa huku akiwaagiza wakurugenzi hao kupeleka taarifa kila mwezi ya mpango wa ujenzi wa madarasa kwa kutumia matofali hayo ofisini kwake.

Kuhusu msaada huo, alisema Plan International inasaidia kujenga utamaduni kwenye jamii wa kuendalea kufanya usafi kwa kunawa mikono ili kuepuka magonjwa ya milipuko kwa kutoa msaada wa vifaa hivyo kwa shule 77 sambamba na kusaidia wanafunzi wa kike kujisitiri wakati wa hedhi.

Awali, Meneja wa Plan International Tawi la Geita, Adolf Kaindoa, alisema vifaa hivyo vina thamani ya Sh. 63,960,000 ambavyo vimelenga kusaidia wanafunzi wa kike kuhudhuria masomo na kukaa darasani bila kuhofia kukosa taulo za kike wakati wa hedhi.

Meneja huyo alisema shirika hilo pia limetoa vifaa vya usafi vikiwamo sabuni za maji, mche na taulo kwa wanafunzi wa kike kwa shule za msingi na sekondari ili kuendeleza utamaduni kwa walimu na wanafunzi wa kunawa mikono muda wote ili kupambana na magonjwa mbalimbali ya kuambukiza.

## ASA yatwishwa jukumu uzalishaji mbegu za pamba

Na Christina Haule, MOROGORO

WAKALA wa Mbegu Tanzania (ASA) imekabidhiwa jukumu la kuzalisha mbegu bora za pamba katika hekta 11.1 zilizoko Igunga mkoani Tabora ili kuongeza uzalishaji na kufikia lengo la serikali la kuanzia kiwanda cha uchakataji wa mbegu mkoani humo.

Kaimu Meneja Uzalishaji wa ASA, Benjamin Mfupe, alisema hayo juzi kwenye Maonyesho ya Wakulima maarufu kama Nanenane Kanda ya Mashariki yaliyofanyika kwenye viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere. Maonyesho hayo yalihusisha mikoa ya Morogoro, Pwani, Tanga na Dar es Salaam.

Alisema serikali imeamua kukabidhi jukumu hilo kwa ASA kwa sababu ndio wanaoshughulika na upatikanaji wa mbegu bora nchini.

Mfupe alisema kwa kukabidhiwa hekta hizo ambazo ni sawa na vijiji 60, watasaidia namna ya kupata mbegu bora, hivyo kuhakikisha uzalishaji wa mbegu unaongezeka huku wakulima wakizipata kwa wakati.

Kwa kutumia mbegu aina ya UKM 08, alisema watahakikisha wanawasimamia wakulima kutokana na mashamba hayo kusimamiwa na ASA na kuhakikisha wanafuata kanuni za kilimo ili kupatikana mbegu bora kwa ajili ya kilimo bora.

## SBL yazindua kampeni Serebuka

Na Mwandishi Wetu

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL), imezindua kampeni mpya inayolenga kuwahamasisha Watanzania kufurahia maisha bila kikomo kupitia bidhaa zake zenye chapa ya Serengeti.

Kampeni hiyo inayojulikana kama 'SEREBUKA' inadhaminiwa na chapa mbili maarufu, bia ya Serengeti maarufu kama Serengeti Premium Lager na bia Serengeti Lite, huku ikilenga kuonyesha kuwa Serengeti ni chapa inayowaleta Watanzania pamoja na kuwafanya wafurahia maisha bila kikomo.

Kwa mujibu wa mkuu wa kitengo cha bia wa SBL, Anitha Msangi, kampeni hiyo inakuja na mambo mazuri na ya kusisimua ikiwa ni pamoja na chakula, muziki na michezo.

"Kampeni ya Serebuka ni kwa ajili ya Watanzania wote na inalenga kuwapa nafasi adhimu wateja wetu kufurahia maisha na bidhaa zetu. Tutakuwa na mashindano ambayo yataongozwa na mastaa mbalimbali wataokuwa wanawaburudisha na kuwafurahisha wateja wetu katika kipindi chote cha kampeni," alisema Anitha

Alisema washindi watashinda zawadi lukuki ikiwamo fedha taslimu shilingi milioni moja.

Wanasiasa wasiowajibika walivyochokwa Pemba

Ukurasa 13





Ukurasa 14

## KENETH KAUNDA: Mkombozi pekee anayeishi Afrika Mkapa alisaidia kumtoa gerezani

siasa

JUMATANO JAGOSTI 12, 2020

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

# Mkapa alikuwa mwanastratejia hodari na muumini halisi wa Nyerere

- Mwalimu hakumpendelea Ben 1995
- Kampeni yetu haikumwogopa Mrema
- Hakuna njia ya kutomteua JK kuwa Waziri
- Hakuniteua kuwa meneja wa kampeni

**Na Waandishi Maalum**

JANA tulichapisha sehemu ya kwanza ya ushuhuda wa FERDINAND Kamuntu Ruhinda, rafiki wa karibu wa Hayati Benjamin William Mkapa, Rais wa Tatu wa Tanzania, aliyefariki dunia Julai 23, mwaka huu, na kuzikwa Julai 29 kijijini kwao Lupaso, Mtwara. Hii ni sehemu ya pili ya ushuhuda wa Mzee Ruhinda, Mwandishi wa Habari, Mshauri na Mwanastratejia wa Siasa, Mhariri na Balozi wa Tanzania katika nchi za Canada na China. Urafiki wa wazee hao wawili ulidumu kwa zaidi ya miaka 50. Sasa endelea kusoma.........

Hata hivyo, tulikubaliana kuhusu mambo mengi. Jambo moja ambalo tulikubaliana wakati wote ni kuhusu Muungano na muundo wake. Tulikubaliana kuwa nchi yetu haikuwa na msisitizo wa kutosha kuhusu Muungano. Pamoja na kwamba nchi yetu ni wamoja sasa, bado kuna watu wengi ambao bado wanazo hisia za Uzanzibari na Utanganyika. Tunahitaji kuongeza nguvu katika kubadilisha hisia hizi kwa sababu nchi hii sasa ni moja. Zilikuwa nchi mbili mwaka 1964, miaka 56 iliyopita."

Anaongeza kwa nini ameteua kulisisitiza jambo hili. "Nalisema hili kwa sababu ni jambo muhimu sana kwa ustawi wa taifa letu na hii ni mara yangu ya mwisho kufanya mahojiano na waandishi wa habari."



Mkapa akipata heshima za kikabila katika moja ya mikoa aliyotembelea.

"Kwangu mimi siyo tu kwamba Benjamin Mkapa alikuwa rafiki yangu. Lakini nimeishi naye, na nimeshuhudia na nilizipenda tabia zake nzuri na sifa zake nyingi. Aliongozwa sana na utu. Alikuwa mpole. Kweli, pia alikuwa mkali, lakini hizo zote ni tabia nzuri tu za binadamu. Hata ukali siyo tabia mbaya, hasa ikiongozwa na utu, upole na haki, kama ilivyokuwa kwa Benjamin Mkapa. Aliongoza nchi vizuri na kwa misingi thabiti ya haki."

Mzee Ruhinda pia anazugumzia suala jingine ambalo Mzee Mkapa alilizungumzia katika kitabu chake, "utawala wa nchi yetu na misingi ya chaguzi zetu."Siku zote, mjadala umekuwa kuhusu umuhimu wa kuwepo kwa Tume Huru ya Uchaguzi. Kwangu mimi, suala kubwa siyo kuwepo ama kutokuwepo kwa Tume Huru ya Uchaguzi, bali muhimu ni kuwepo kwa chombo ama vyombo vinavyoaminiwa na wananchi na jamii, vilivyojengwa katika misingi ya utamaduni wetu, ili chaguzi zetu zikubaliwe na wananchi, zidumishe amani, na zisilete misuguano katika jamii."

Anafafanua, "Hili ndilo jambo la msingi. Kuwapo kwa chaguzi za haki na zinazokubaliwa na wananchi, kwa sababu hata huko Nchi za Magharibi hakuna kitu kinachoitwa Tume Huru za Uchaguzi. Lakini utamaduni wa nchi hizo, umejengeka kiasi cha kuruhusu chaguzi zao kukubaliwa na wananchi na matokeo ya chaguzi hizo kutokuzusha mivutano isiyokuwa ya msingi."

Maoni yangu, anasema Mzee Ruhinda, ni wajibu wa Tume ya Uchaguzi kufanya kazi vizuri na kwa uwazi, na kujenga mazingira ya chaguzi za haki ambako wananchi wanapata taarifa nzuri, za kutosha na kwa wakati.

"Chukua mfano wa uchaguzi mkuu wa mwaka 1995, uchaguzi mkuu wa kwanza baada ya siasa za vyama vingi kurejeshwa nchini. Wakati wa kampeni ya uchaguzi ule, uliandaliwa mdahalo baina ya wagombea. Lakini mdahalo ule uliandaliwa na gazeti moja, na wala siyo na Tume ya Uchaguzi," anasema Mzee Ruhinda na kuongeza:

"Lakini tokea wakati ule, haujapata kuandaliwa Mdahalo mwingine, na kwa maoni yangu, hiyo ni sehemu muhimu ya kazi za Tume ya Uchaguzi, yaani kuwawezesha wananchi wawajue vizuri wagombea wao, misimamo yao kuhusu masuala mbalimbali na maandalizi yao ya kuongoza nchi. Uwazi wa namna hiyo utasaidia kujenga mazingira ya chaguzi zetu kuaminiwa zaidi na wananchi."

Anamalizia Mzee Ruhinda: "Napenda nimalizie kwa kutoa tena pole nyingi, na rambirambi za dhati ya moyo wangu, kwa familia ya Ben Mkapa - kwa mama na watoto na wajukuu na ndugu zake wote - na pia kwa marafiki zake wengi na wote. Nimefurahishwa na jinsi taifa letu lilivyomuaga na tulivyomsindikiza Ben Mkapa. Ameagwa kwa heshima na taadhima. Kwangu mimi, I will miss him. I will miss him very much!

Balozi Ruhinda alistaafu serikalini, kutoka Wizara ya Mambo ya Nje, mwaka 1993, akiwa Balozi wa Tanzania nchini China na kurejea nyumbani. Mwaka 1994, aliombwa kuyasaidia kitaaluma magazeti ya Business Times la Kiingereza na Majira la Kiswahili.

Kwa maana nyingine, Mzee Ruhinda alistaafu wakati mwafaka kabisa, kabla ya vuguvugu la uchaguzi mkuu wa 1995, wakati Rais Ali Hassan Mwinyi akimaliza muda wake wa uongozi na taifa likijiandaa kumchagua rais wa tatu.

Anaelezea mwenyewe Mzee Ruhinda: "Mwaka ule wa 1995, wagombea walikuwa wengi, na kila mgombea alikuwa na kundi la waliomuunga mkono tokea mwanzo. Kwa upande wa Mkapa, tulikusanyika watu wachache, marafiki zake wa karibu wa kisiasa na kikazi. Walikuwepo Hashim Mbita, Walter

INAENDELEA UK.12

# Mkapa alikuwa mwanastratejia hodari na muumini halisi wa Nyerere

INATOKA UK.11



Akiyekuwa Rais wa Marekani, Bill Clinton (kushoto) pamoja na Mkapa, kwenye moja ya majukwaa ya kimataifa jijini Dar es Salaam. **PICHA: WAANDISHI MAALUM.**

Bgoya, Balozi Saleh Tambwe, Balozi Suleiman Hemed, Patrick Quorro na Mateo Quaresi...."

Kwa sasa Mbita, aliyekuwa Katibu Mtendaji wa Kamati ya Ukombozi ya Afrika, Patrick Quorro, aliyepata kuwa mbunge na Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa TANU na Balozi Hemed ni marehemu. Walter Bgoya ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Uchapishaji Vitabu ya TPH, iliyochapisha vitabu vyote vya Mzee Mkapa, Balozi Tambwe pamoja na Mateo Qaresi, aliyepata kuwa mbunge na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, ni wamestaafu.

Anaelezea Balozi Ruhinda: "Mwanzoni, hatukujipanga vizuri, tulikuwa 'disorganized' kidogo hivi. Kuona hivyo, Hashim Mbita katika mikutano yetu ya mwanzo, alipendekeza niwe 'coordinator' mratibu wa kundi hilo na shughuli ya kampeni kwa jumla. Hivi ndivyo niliishia kuwa msimamizi wa ofisi binafsi ya mgombea urais na meneja wa kampeni ya Mkapa mwaka ule, hakuniteua kuwa meneja wa kampeni yake. Ni mazingira yaliyoniweka katika nafasi hiyo."

Mzee Ruhinda ambaye alikuja pia kuifanya kazi hiyo hiyo wakati Jakaya Kikwete akigombea urais kwa mara ya pili mwaka 2005 na akashinda, anaielezea kazi ya kampeni ya mwaka 1995.

"Kazi ile ya kampeni ilikuwa ngumu sana. Makao makuu ya CCM yalikuwa kama yameisusa. Nadhani kwa sababu mbili. Kwanza, ushiriki na mchango wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, katika mchakato wa kumpata mgombea wa CCM mwaka ule, ulikuwa umekiacha chama hoi sana....kama vile kimepigwa na bumbuazi na ganzi. Pili, wagombea wote ambao walikuwa wanapendelewa na CCM makao makuu walikuwa wameshindwa kwenye mchakato huo. Hivyo, kampeni yetu ikajikuta inalazimika kusimamia kila kitu, ukiwamo hata uratibu na usimamizi wa safari za kampeni za Mwalimu mwenyewe."

Anaongeza: "Katika nafasi yangu hiyo ya uratibu, tulisafiri na Ben katika hatua za mwanzo za kuwania kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi (CCM) kutafuta wadhamini. Tulisafiri kwa treni na mabasi. Tulikwenda mikoa ya Ziwa...tulikwenda naye Tabora, Shinyanga, Mwanza na Kagera kabla haijapigwa ile kura ya kwanza ndani ya CCM. Baadaye alisafiri na wenzangu kwenda mikoa ya Kaskazini, na baadaye ya Kusini."

Anafafanua Balozi Ruhinda: "Mwanzoni Ben, hakuwa na 'visibility' kubwa ya kisiasa, kwa maana kuwa hakujulikana sana ...nguvu yake kubwa ilikuwa kwenye mikoa ya kusini kwa sababu alikuwa amekuwa mbunge kule, na watu wengi walimjua na walizijua sifa zake. Kule alikuwa maarufu. Lakini hakuwa na ushawishi mkubwa katika maeneo mengine ya nchi."

"Kuwa ambalo Ben aliwashinda wenzake, wakati huo, ni kwamba alifanya 'homework' yake vizuri. Alifanya uchambuzi wa hali ya nchi, changamoto zake na akabuni majawabu ya changamoto hizo. Alijua nchi na matatizo yake kwa maana ya changamoto za kila kanda."

Ruhinda pia anafafanua kuhusu mchango wa Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, wakati wa hatua za mwanzo za kugombea urais mwaka 1995, na kusisitiza kuwa Mwalimu hakumpendelea Ben kama watu wengi wanavyohisi na hata kutangaza.

"Mwalimu hakumpendelea Ben, hata kidogo, katika hatua zile za mwanzo. Siamini, na najua kuwa Ben hakuwa mgombea chaguo la Mwalimu, aliacha uwanja wazi na kuachia ushindani ufanye kazi yake. Alichokuwa nacho Mwalimu wakati huo, na alikisema mara nyingi, tena hadharani, ni sifa kuu za mgombea urais wa Tanzania mwaka ule wa 1995," anaelezea Mzee Ruhinda na kuongeza:

"Isitoshe, ilijulikana wakati huo kuwa chaguo hasa la Mwalimu la mtu wa kuwa rais wa tatu wa Tanzania, alikuwa ni Salim Ahmed Salim, ambaye wakati huo alikuwa mjini Addis Ababa, Ethiopia, kwenye nafasi yake ya ama Katibu Mkuu wa Umoja wa Afrika (OAU) au Uenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AU). Sijui kama jina na shabaha za chombo hicho zilikuwa zimebadilika tayari. Kwa sababu ambazo sijapata kuzielewa wala kuziulizia, Salim alisita kuweka jina kwenye kinyang'anyiro na hivyo kuacha uwanja wazi kwa wengine."

Anaongeza : "Na kwa sababu ya 'visibility' yake ndogo katika siasa za hapa nchini, kura alizopata Ben ziliwashangaza wengi katika vikao vya uteuzi vya CCM. Kama nilivyosema, nguvu yake ilikuwa katika kufanya 'homework' na uchambuzi wake vizuri wa hali ya kisiasa nchini. Hivyo, wakati wagombea watatu wa mwisho - Ben mwenyewe, JK na Cleopa Msuya, wanaingia katika tatu bora kupigiwa kura na Mkutano Mkuu, kila mgombea alionekana kuwa nafasi sawa."

"Nadhani mtakuwa mnakumbuka; katika kura ya kwanza ya Mkutano Mkuu, JK alipata kura nyingi kuliko wenzake wawili. Alikuwa na kundi kubwa ya vijana. Lakini hakuna mgombea aliyepata asilimia 50 ya kura. Hivyo, Kamati Kuu iliamua kuwa kura zirudiwe kati ya wagombea wawili wa kwanza, ili apatikane mshindi mwenye 'majority' badala ya 'plurality'...Cleopa Msuya aliondolewa wakabakia Ben na JK," anasema na kuongeza:

"Katika kura ya pili na ya mwisho, Ben alishinda kwa kupata kura zaidi kidogo, lakini ukweli ni kwamba wagombea wote wawili walikuwa karibu na nguvu sawa ya uungwaji mkono miongoni mwa wajumbe. Ilikuwa baada ya kupatikana mgombea rasmi wa CCM, ndipo Mwalimu Nyerere aliingia rasmi katika kampeni za uchaguzi mkuu kutafuta Rais wa Tanzania. Na Mwalimu Nyerere aliingia kati kwa sababu alikuwa ameridhishwa na jinsi mchakato wa kumpata mgombea urais ndani ya CCM ulivyokuwa umeendeshwa."

Ruhinda pia anazungumzia kampeni za uchaguzi mkuu wa 1995 na upinzani kutoka mgombea wa NCCR-Mageuzi, Augustine Mrema na jinsi kampeni ya Mkapa ilivyomchukulia mpinzani wao huyo:

"Uchaguzi wa mwaka 1995 ulikuwa wa kwanza wa vyama vingi baada ya mabadiliko ya sera nchini. Kweli, ulikuwa uchaguzi wa ushindani, lakini hatukumwogopa Mrema. Kwa sisi tuliofahamu vizuri, tokea akiwa Waziri, na kumfanyia uchambuzi wa kutosha, tulimjua vizuri. Kwetu sisi, alikuwa mgombea mwepesi kidogo."

Anasisitiza: "Na kweli Tanzania ya wakati ule, na nadhani ya wakati wowote, ilihitaji Rais makini, aliyeijua nchi na changamoto zake, aliyeijua dunia na jinsi inavyoendeshwa na kufanya kazi. Hata vyombo vya habari makini viliujua ukweli huo."

Anaongeza: "Kwa maoni yangu, mambo mawili yalimmaliza Mrema. Yote mawili kwa sababu Mwalimu kuingilia kati kwenye kampeni. Kwanza, ilikuwa ni hotuba zake za pale Mbeya na Kilimanjaro, akielezea aina ya kiongozi wa Tanzania aliyefaa wakati huo na aliyezijua fika changamoto kuu za nchi yetu, rushwa, ukabila, Uzanzibari na Utanganyika, na mambo mengine. Nadhani hizi hotuba mbili bado ni muhimu sana, na inafaa zichapishwe, ili watu waendelee kuzisoma milele, na watu kujua alichokisema Mwalimu, kwa sababu changamoto zile bado zipo mpaka leo."

"Pili, ilikuwa hotuba ya Mwalimu pale Jangwani, Dar es Salaam, wakati tunamaliza kampeni. Mwalimu hakumtaja Mrema kwa jina, lakini alimdhihaki kweli kweli. Alisema kuwa kama mtu anataka kubebwa, na watu wa kumbeba wapo, basi waendelee tu kumbeba...maneno mengine sitaki kuyarudia. Kwa jumla, Mrema alikuwa mgombea mwepesi. Kweli, alipata asilimia 27 ya kura. Hizi zilikuwa kura nyingi katika mazingira ya wakati huo, lakini kwa kweli hakuwa mgombea makini sana."

Mzee Ruhinda anasema kuwa kampeni ile ya mwaka 1995, na nyingine ambayo pia aliisimamia kama Meneja ya mwaka 2005, wakati JK anagombea kwa mara ya kwanza, zilizidi kumsukuma karibu na wanasiasa kwa maana ya kupanua wigo wa watu aliowajua, na alioweza kuwashauri, hata kama kweli amekuwa mwanaharakati wa siasa miaka yote.

"Nimewashauri mambo mengi wanasiasa. Mengi nilishauri waliyakubali. Hata hivyo, yapo waliyoyakataa ama kuyatekeleza. Moja ni kuhusu tabia na mwenendo wa wanasiasa hao kuiita CCCM chama tawala. Niliwaambia kuwa tabia ya kuiita CCM chama tawala ilikuwa inajenga mazingira ya kuonekana kama chama dola. Ukweli ni kwamba CCM ni chama cha wanachama . Lakini, nadhani, nilishindwa kuwashawishi wanasiasa kuhusu jambo hilo. Linawavutia sana, sijui kwa nini?"

Ruhinda pia alizungumzia kuhusu uundwaji wa serikali ya kwanza ya Ben na uamuzi wake wa kumshirikisha mshindani wake mkuu wa urais ndani ya CCM, JK katika serikali kwa kumteua kuwa Waziri wa Mambo ya Nje. Anasema:

"Benjamin Mkapa, kwa fikra, elimu, uzoefu na maisha, alikuwa mwanastratejia (strategist). Kwanza yeye na JK walikuwa wamefahamiana miaka mingi wakati Jakaya alipokuwa Katibu wa CCM wa Wilaya ya Masasi, na Ben alikuwa mbunge kule. Kwa hiyo, Ben alikuwa anamjua vizuri Kikwete na walikuwa wametumikia pamoja katika Baraza la Mawaziri la Rais Mwinyi."

"Zaidi ya hapo, Kikwete, mwaka ule wa 1995, alikuwa na nguvu nyingi, ushawishi na uungwaji mkubwa wa vijana, walikuwa ni nguvu kubwa. Ben kama mwanastratejia asingeweza kumwacha nje ya serikali yake mtu wa namna hiyo. Ni lazima umchukue uwe nawe. Sababu nyingine za uteuzi huo, mimi sizijui."

Sasa baada ya kazi kubwa ya kuendesha kampeni ya uchaguzi mkuu yenye mafanikio makubwa, kwa nini basi Mkapa hakupata kumteua Balozi Ruhinda kwenye nafasi yoyote ndani ya serikali yake? Balozi anacheka kidogo kabla ya kujibu swali hili.

"Ukweli ni kwamba sikupata kumwomba kazi naye hakupata kunipa kazi. Ningeweza kuomba kazi, na yeye asingeniniyima; na yeye angeweza kunipa ofa ya kazi, na mimi nisingekataa. Nikilifikiria jambo hilo na hali hiyo leo, nadhani msimamo wetu ulikuwa murua, wa busara na mwafaka kabisa. Ilituwezesha kubakia na kuendelea na urafiki wetu wa karibu."

Anaongeza kuwa pengine angekubali kupewa wadhifa fulani katika serikali ya Mkapa "ningeshindwa kutekeleza baadhi ya majukumu yangu, kwa sababu ya huu urafiki".

Kukataa kwa Ferdinand Ruhinda kuomba na kupewa kazi katika serikali ya rafiki yake na msimamo wa Ben kutomlazimisha rafiki yake amsaidie kwenye serikali yake mpya ni uthibitisho mwingine wa aina ya viongozi hao wawili, yaani watu wasiohangaishwa na vyeo, wala kujikweza kupitia vyeo vya kiserikali.

***Makala hii imeandikwa na waandishi waandamizi nchini. Salva Rweyemamu na Saidi Nguba ambao kwa sasa wanaongoza Kampuni ya Mawasiliano ya Pioneer Communications na Tido Mhando Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya habari ya Azam Media. Usikose sehemu ya tatu na ya mwisho ya Makala hii: Falsafa iliyoongoza Sera za Serikali ya Mkapa. Kwa nini alisimamia ubinafsishaji? Kwa nini alikataa kuifanya Serikali iwe yake binafsi? Kwa nini alikataa tashihisi (personification) na alichukizwa na tabia ya kumtukuza yeye binafsi? Kwa nini Benjamin Mkapa alikuwa mwandishi wa habari halisi na mhariri makini?***

# Wanasiasa wasiowajibika walivyochokwa Pemba



Wanachama wa Pemba Youth Organisation katika majadiliano ya uwajibikaji kwenye mkutano na wanahabari.
**PICHA: MWANDISHI WETU.**

**Na Mwandishi Wetu**

UPO msemo wa Waswahili kuwa alalaye usimwamshe kwani ukimwamsha utalala wewe, lakini kwa wanasiasa ni vyema kuwaamsha wanapolala kwa vile wasipozinduka, wapigakura wao watakosa wa kuwasemea iwe majimboni au kwenye kata ambazo waliyemchagua anakoroma usingizini.

Huo ndiyo ujumbe unaotumwa kwa wanasiasa wanaotarajia kuingia kwenye uwanja wa ubunge na uwakilishi wakati pazia la kampeni likifunguliwa mwezi huu. Wapigakura wanawataka wawajibike kwani wanaona kuwa hakuna uwajibikaji wa kutosha na wanasiasa hao hawaonekani majimboni.

Hivi karibuni Nipashe ilizuru Pemba na kuzungumza na baadhi ya vijana wilayani Wete ambao wanalalamikia viongozi kutokuwajibika kwa wapiga kura.

Wanawakosoa wawakilishi na wabunge wao kuwa wanachowafanyia baada ya kuwachagua ni uwajibikaji usioridhisha na kujiweka mbali na masuala au changamoto za kijamii kwenye majimbo yao.

Kwa mfano, wanaeleza jinsi wanafunzi wa shule za msingi sehemu nyingi za Pemba wanavyokwamishwa masomo

na tatizo la ukosefu wa vyoo, wanadai si viongozi wala wawakilishi na wabunge waliotayari kuwatatulia watoto wa wapigakura wao tatizo hilo.

Katibu wa asasi ya kiraia ya 'Pemba Youth Organisation' inayohamasisha kujitambua, kuondokana na umaskini na unyanyasaji wa kijinsia, Rukia Ibrahim Kombo, katika mijadala ya wanahabari, anasema mojawapo ya mambo ambayo waliyasimamia na kuyadai ni vyoo bora kwa wanafunzi wilayani hapo, lakini hakuna mafanikio.

Anasema katika mradi wa afya shuleni walihamasisha ujenzi wa vyoo bora shuleni ili mabinti na wanafunzi wengine wasikwame kupata elimu kwa vile baadhi ya shule zilikuwa hazina vyoo na wanafunzi wakijisaidia vichakani na sehemu nyingi shule zilikuwa na msongamano mkubwa chooni.

Anaitaja sera ya elimu inayoelekeza kuwa wanafunzi 20 wa kike kutumia choo au tundu moja na kwa wanaume ni 25 kwa kila tundu lakini walipofanya utafiti walibaini kuwa kulikuwa na upungufu wa kutisha kwani zaidi ya wanafunzi 200 walikuwa wanatumia tundu moja la choo.

Anasema walifanya kampeni kupitia mitandao ya kijamii lakini hakuna hatua iliyochukuliwa licha ya viongozi wao kuwa mojawapo wa walengwa waliokuwa wanatumiwa ujumbe mara kwa mara.

Saada Saleh mwanachama wa asasi ya Vijana Wanawake Pemba ambaye alitaka kuwa mbunge wa jimbo la Kojani kwa tiketi ya CCM, anasema ukosefu wa vyoo shuleni

> "Hakuna sehemu ya kujisitiri wala kujifanyia usafi, vyoo ni vibovu au vimejaa na mazingira hayo si rafiki kwa wasichana." Anaeleza.

sehemu nyingi kisiwani Pemba si jambo jipya.

"Kuna mambo mengi ya kushughulikia shule za jimbo la Kojani, kwa mfano nyingi hazina vyoo, hata vilivyoko ni vibovu na vimejaa, si jambo geni ni matatizo ambayo yapo." Anasema Saada ambaye hata hivyo hakupitishwa kuwa mgombea ubunge kwenye hati za awali.

Licha ya kuondolewa kwenye mchujo, muonyesha nia huyo anasema ukosefu wa vyoo bora umekwamisha mabinti wengi Pemba kusoma, kwa mfano wanapokuwa katika hedhi na kwamba hata yeye tatizo hilo lilimsumbua pia.

"Hakuna sehemu ya kujisitiri wala kujifanyia usafi, vyoo ni vibovu au vimejaa na mazingira ni hayo si rafiki kwa wasichana." Anaeleza.

Mkurugenzi wa Wilaya ya Micheweni, Suleimani Juma Pandu, anapoombwa ufafanuzi wa suala hilo hakuwa tayari kulizungumzia.

Pandu ambaye awali alikuwa wilaya ya Wete na sasa yuko Michewezi anakataa kueleza jitihada za kujenga vyoo kwa madai kuwa hayuko tayari kuzungumzia taarifa za serikali kwa simu.

VIONGOZI HAWAWAJIBIKI

Pamoja na masuala ya afya na elimu, vijana wanazungumzia usiri kwenye upatikanaji wa taarifa fedha za maendeleo ya ambazo waamini ni kodi za wananchi na wanahitaji kufahamu, wanataja mifuko ya maendeleo ya jimbo wanayopata wawakilishi na wabunge.

Wanaeleza kuwa ni vigumu kufahamu matumizi ya fedha hizo wala kufuatilia iwapo vijana nao wanaweza kufahamishwa namna watakavyofaidika.

Vijana wanataka kuwafikia wabunge na kuzungumzia kuhusu fedha hizo na jinsi zinavyoweza kuwa na ongezeko la thamani kimaendeleo lakini ugumu unaowakwamisha ni wawakilishi wao hawafikiki, kwani wawakilishi na wabunge hawaonekani majimboni kwa muda mrefu licha ya kwamba walitakiwa kuwa karibu na wapigakura wao.

Kwa upande mwingine vijana wanawakosoa wapinzani ambao kwa miaka mingi licha ya kuwa wawakilishi na wabunge wa Pemba, hawajafanya juhudi za kutosha za kusaidia kuboresha maisha ya wananchi.

Wanalalamika kuwa wabunge wakishachaguliwa hawaonekani majimboni lakini wakati wa kampeni wanarudi kuwapigia magoti na kuomba kura.

Wanasema wagombea wakipata uongozi wanahama na ni kwa nadra wanaonekana Pemba, pengine siku ya kurejea baada ya kuapishwa bungeni lakini baada ya hapo hawaonekani.

Adha, wananchi hawazifahamu taarifa za fedha za mifuko hiyo na hakuna mbunge au mwakilishi anayewaelezea wapigakura kuhusu fedha na uwepo wa mifuko hiyo na namna wanavyoweza kufaidika nayo.

Hata hivyo, vijana hao wanawakosoa wabunge na wawakilishi wao kuwa hawajawajibika vya kutosha kuwahudumia wananchi licha ya kwamba Pemba kwa miaka mingi imekuwa na wabunge wa CUF lakini hawajafanya kile wananchi walichokuwa wakikitamani.

Musa Said Suleiman, ni mwezesha wa kijamii anayefanyakazi za kuhamasisha mabadiliko, anazitaja chokochoko na chuki za kisiasa kama kuegemea zaidi itikadi za kichama kwa mfano 'mimi ni wa mrengo wa chama hiki , siitambua serikali ya chama flani wala simuungi mkono mbunge au mwakilishi wa chama flani' kuwa ni miongoni mwa matatizo yanayowasumbua wapigakura ambao wanashindwa kuwafikia na kuwahoji viongozi wao wa kisiasa.

Kwa upande mwingine vijana hao wanashauri kuwe na uwakilishi mpana zaidi kwenye idadi ya wajumbe wanazisimamia na kuzipangia matumizi fedha za mfuko wa maendeleo ya jimbo za wabunge na wawakilishi ili kuongeza uwajibikaji katika kuzisimamia na kuwaletea wananchi maendeleo kwani kwa sasa ni wachache wanaofahamu habari za mifuko hiyo ya kuchochea maendeleo.

Suala la wabunge na wawakilishi kukosa ofisi nalo linaibuliwa . Vijana wanasema hawana ofisi hivyo inakuwa vigumu kuwafikia, serikali ya awamu ijayo ijenge miundombinu hiyo.

# KENETH KAUNDA: Mkombozi pekee anayeishi Afrika

- Mkapa alisaidia kumtoa gerezani

Na Mwandishi Wetu

KENNETH David KAUNDA maarufu kama KK ndiye mpigania uhuru pekee anayeishi barani Afrika baada ya mababa wa ukombozi waliolitoa bara hili kwenye ukoloni mkongwe kufariki dunia.

KK aliyezaliwa Aprili 28, 1924 alikuwa Rais wa kwanza wa Zambia, aliyelitumikia taifa hilo kuanzia mwaka wa 1964 hadi 1991.

Mpigania uhuru na mwanamapinduzi wa Afrika na Baba wa Taifa la Zambia anasimama na kubakia kuwa nguzo ya umoja na shujaa wa uhuru Afrika.

Sifa za KK ni pamoja na utu, ubinadamu, ujasiri, huruma, msimamo, weledi, unyenyekevu, ushawishi, ucha Mungu na uchapakazi. Si mtu wa kujilimbikizia mali pengine ni kiongozi fukara licha ya kuiongozi Afrika na Zambia kipindi ambacho marais wa bara hilo akiwamo Mobutu Sseseko wa Zaire walijilimbikizia mali kwa kufuru.

Anatajwa kuwa ametimiza jukumu kubwa la kuupigania uhuru wa Zambia na ukanda wa Kusini mwa Afrika.

### UHURU WA ZAMBIA

Mapambano ya uhuru nchini humo yalianza mwaka 1949, wakati huo kama alivyofanya Mwalimu Julius Nyerere, KK naye alijiuzulu kutoka ualimu wa shule ya msingi na kujikita katika masuala ya siasa kwa nguvu na kasi zaidi kupigania uhuru wa taifa lake.

Baada ya kutumikia nafasi mbalimbali akishika nyadhifa kadhaa ndani ya chama ambacho alikuwa mwasisi na Kaunda alichaguliwa kuwa rais wa kwanza wa chama cha ukombozi cha Zambia's United National Independence Party (UNIP) mwaka 1960, baada ya kuachiwa kutoka kifungoni.

Baada ya miaka mine ilipofika 1964 Zambia ilipata uhuru wake kutoka kwa Waingereza . Koloni hilo lilijulikana kama Northern Rhodesia na KK akawa rais wa kwanza wa taifa hilo baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 1964.

Aliendelea kulitumikia taifa hilo hadi ilipotimia miaka 27 alipoangushwa na Frederick Chiluba aliyeingia madarakani kwa chama cha upinzani cha Movement for Multi-Party Democracy mwaka 1991.

Afrika imebakiwa na mwanamapinduzi pekee Keneth Kaunda.

### MAISHA YA AWALI

Kaunda ni mtoto wa mwisho katika familia ya watoto wanane. Alizaliwa katika hospitali ya Misheni ya Lubwa katika kitongoji cha Chinsali, katika Mkoa wa Magharibi mwa Northern Rhodesia ambayo sasa ni Zambia.

Baba yake alikuwa mmishenari Mchungaji David Kaunda, kutoka taifa jirani la Malawi aliyekuwa kiongozi na mwalimu wa shule za wamishenari. Alihamia Chinsali kwa lengo la kufanya kazi katika misheni ya Lubwa.

### MASOMO

Alianza masomo kadhaa katika kituo cha Munali Training Centre ya mjini Lusaka kuanzia Agosti, 1941 hadi 1943.

Kaunda pia aliwahi kuwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi na bweni ya Upper Primary School kuanzia mwaka wa 1943 hadi 1945. Alianza kazi ya ualimu huko Lubwa na kuelekea zake mjini Lusaka kwa lengo la kuwa ofisa mwelekezi wa jeshi.

Kuna wakati alikuwa akifanya kazi katika migodi ya Salisbury na Bindura nchini Afrika Kusini na mnamo mwaka wa 1948, alikuwa mwalimu katika shule ya mjini Mufulira ya United Missions to the Copper belt (UMCB).

Aidha, aliwahi kuwa msaidizi katika Kituo cha Ustawi wa Jamii wa Afrika na Bodi ya Walimu wa Shule ya Mine School ya mjini Mufulira.

### KUANGUSHWA NA UPINZANI

KK anakuwa kiongozi wa kwanza miongoni mwa wapigania uhuru wa Afrika kuondolewa ikulu na wapinzani kwenye uchaguzi mkuu.

Novemba 2, mwaka, 1991 gazeti la Telegraph la Uingereza liliripoti kuwa rais wa Zambia Kenneth Kaunda, amekuwa kiongozi wa kwanza wa kupigania uhuru na baba wa taifa linalozungumza Kiingereza kuondolewa madarakani kwa amani baada ya kukubali kushindwa na mpinzani wake.

Aliyemwangusha Kaunda ni Fredrick Chiluba katika uchaguzi mkuu wa mwaka 1991.

Kaunda anaelezwa kuwa hakutokwa na machozi, aliposhindwa na Chiluba, Lakini mmoja wa wanasiasa wa chama chaka Rupia Banda, aliposhindwa na Michael Sata mwaka 2011, hakuwa na hiana aliliambia taifa kwamba: "Sina kinyongo moyoni mwangu." Namtakia kila la kheri wakati wa muhula wake wa urais. Muda wangu umekwisha, ni wakati kwangu kusema kwaheri." Pengine alimuiga Dk. Kenneth Kaunda.

### KUTUPWA GEREZANI

KK alitoka madarakani Novemba 2, 1991 baada ya Chiluba kuingia madarakani kupitia chama cha Movement for Multiparty Democracy. Baadaye askari waasi walitaka kumpindua Rais Chiluba.

Kutokana na tukio hilo alimkamata Kaunda wakati huo akiwa na miaka 73, Chiluba akimtuhumu kujihusisha na jaribio la mapinduzi. Kaunda alikana kuwa na uhusiano na askari waliotaka kumpindua Rais Chiluba.

Akiwa madarakani, Rais Chiluba alishinda jaribio la kutaka kupinduliwa na wanajeshi waasi na ndipo aliwakamata viongozi kadhaa wa upinzani akiwamo Kaunda akiwatuhumu kuhusika na upangaji njama wa kufanya mapinduzi.

> Baada ya kutumikia nafasi mbalimbali akishika nyadhifa kadhaa ndani ya chama ambacho alikuwa mwasisi Kaunda alichaguliwa kuwa rais wa kwanza wa chama cha ukombozi cha Zambia's United National Independence Party (UNIP) mwaka 1960, baada ya kuachiwa kutoka kifungoni.



Kenneth David Kaunda

### KUTOKA GEREZANI

Baada ya kifo cha rais mstaafu Benjamin Mkapa ilidhihirika kuwa mwaka 1997 akifanya kazi nchini Zambia akiwa ofisa wa ubalozi, Krismasi ya mwaka huo 1997, serikali ya Zambia ilimkamata Mzee Kenneth Kaunda na kumuweka gerezani.

Suala hilo lilizua kizaazaa karibu dunia nzima na wengi wanajua jinsi Mwalimu Nyerere alivyokuja kuwezesha Mzee Kaunda atoke gerezani, anasema Balozi wa Tanzania nchini Israeli Job Masima.

Na katika maisha yake Mwalimu aliingia gerezani katika gereza lililoko mji wa Kabwe nchini Zambia na baadaye Kaunda akatoka.

"Kitu watu wasichofahamu ni kwamba ingawa kweli Mwalimu alikuja na kucheza mchezo wa mwisho, shughuli yote aliifanya Mzee Mkapa. Ndiye aliyewasiliana na Frederick Chiluba.

"Mzee Mkapa ndiye aliyemtafuta Mwalimu na kumshawishi aingilie kati," anasema Balozi Masima. Mkapa aliyemwezesha Mwalimu Nyerere kwa usafiri na huduma nyingine za kumfikisha mpaka gerezani. Mkapa alifanikisha kupatanisha viongozi wa nchi moja, waliokuwa na tofauti kutokana na vyama tofauti ."

MITANDAO



# Ajira milioni 6 zatolewa kwa miaka mitano

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema kwa kipindi cha miaka mitano serikali imetengeneza zaidi ya ajira milioni sita kupitia sekta mbalimbali ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya kimkakati.

Majaliwa alisema hayo juzi alipokuwa akifungua Mkutano Mkuu wa Kwanza wa Jumuiya ya Wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu (TAHLISO), uliofanyika jijini hapa.

Alisema moja ya ahadi za serikali ya awamu ya tano ilikuwa kukuza uchumi pamoja na kukabiliana na ukosefu wa ajira.

Waziri Mkuu alibainisha kuwa kupitia sekta za viwanda, kilimo, biashara, madini, utalii, miundombinu ya kimkakati na mifumo ya mikopo nafuu, zimezalishwa ajira za kutosha kwa Watanzania.

Alifafanua kuwa, kupitia ujenzi wa viwanda vipya, ajira 482,601 zimetengenezwa huku kupitia utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati kukiwa na ajira 6,032,299.

**Aidha, kwa yale yaliyopo lakini hayafanyi kazi nayo yafufuliwe ili kukabiliana na changamoto za unyanyasaji wa kijinsia zinazowakumba wanachuo husussan wa kike.**

"Pia kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) zaidi ya Sh. bilioni 935.94 imehawilishwa katika kaya maskini Tanzania Bara pamoja na kutekeleza miradi 8,384 ambayo imezalisha ajira za muda kwa kaya 230,738," alisema.

Majaliwa alisema katika kuongeza wigo wa upatikanaji wa mikopo nafuu kwa wajasiriamali wadogo na wa kati na halmashauri kutenga fedha asilimia 10 kwa ajili ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, zaidi ya Sh. bilioni 93.2 zimetolewa na kufungua ajira binafsi.

"Mifuko mbalimbali ya uwezeshaji ukiwemo Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambao unatoa mikopo yenye riba nafuu kwa vijana katika kila halmashauri ambapo zaidi ya Sh. bilioni 5.4 zimetolewa na kutengeneza ajira zaidi ya 26, 970," alisema.

Alisema Mfuko wa Kuendeleza Wajasiriamali Wananchi umetoa zaidi ya Sh. bilioni 8.1 na kutengeneza zaidi ya ajira 4,471 na Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake umetoa zaidi ya Sh. bilioni 62 na kutengeneza zaidi ya ajira 133,880.

"Kutoa vitambulisho maalumu kwa gharama nafuu kwa wajasiriamali wadogo, ili Watanzania hao wanyonge kuendesha shughuli zao bila ya kubughudhiwa, kwa mfano, zaidi ya wajasiriamali 1,591,085 walipatiwa vitambulisho hivyo," alisema.

Katika hatua nyingine, Majaliwa aliagiza taasisi za elimu ya juu ambazo hadi hivi sasa zimekosa madawati ya jinsia, zianzishe madawati hayo mara moja.

"Aidha, kwa yale yaliyopo lakini hayafanyi kazi nayo yafufuliwe ili kukabiliana na changamoto za unyanyasaji wa kijinsia zinazowakumba wanachuo husussan wa kike," alisema.



Wafanyabiashara wa zabibu wakijaribu kumshawishi mteja anunue bidhaa zao, nje ya soko kuu la Majengo, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. Fungu moja linauzwa kwa bei ya 500/- hadi 2,000/- kulingana na ubora wake. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Wadau wa ngozi watakiwa kuchangamkia fursa viwanda

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imewataka wadau wa ngozi nchini kuchangamkia fursa ya uwapo wa kiwanda cha kuchakata ngozi kinachojengwa jijini Dodoma kuzalisha bidhaa mbalimbali zitokanazo na ngozi.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhandisi Stella Manyanya, alisema hayo juzi alipofanya ziara ya kutembelea na kukagua kiwanda hicho jijini hapa.

Manyanya alisema kuwa mradi huo ukikamilika eneo hilo litakuwa kijiji cha ngozi hivyo ni wakati sahihi wa wadau wa ngozi kujitathimini na kuhakikisha ngozi zinafikishwa kwenye kiwanda hicho ili kutengeneza bidhaa zitokanazo na ngozi.

"Sisi matarajio yetu, serikali itatenga fedha kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati hivyo wadau tunataka tushirikiane katika dira hii ili kufanya kitu cha uhakika na kuhakikisha viatu na bidhaa nyingine zinazopatikana kwenye ngozi zinakuwa zinazalishwa hapa nchini," alisema.

Manyanya alisema kuwa ngozi itapatikana kutoka katika maeneo mengine hapa nchini.

"Hivyo basi niwatake wadau sekta ya ngozi kwa kuwambia mambo yameiva, sasa ni wakati wa kuchangamkia fursa zilizopo makao makuu ya nchi Dodoma," alisema.

Aliagiza kiwanda hicho kujengwa kwa ubora unaohitajika , kusimamiwa vizuri ili kupata jengo bora, na matumizi ya fedha yaendane na ubora wa jengo.

# Waandishi wafundwa kujikinga na corona

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAANDISHI wa habari wametakiwa kuendelea kujikinga dhidi ya maambukizi ya virusi vya corona kwa kuzingatia miongozo inayotolewa na wataalam wa afya.

Akitoa mada jana kwa niaba ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Francis Lutalala, kwenye mafunzo yaliyotolewa na Chama Cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Dodoma (CPC) na Umoja wa Klabu za Habari nchini (UTPC), alisema waandishi wanatakiwa kufuata miongozo hiyo kutokana na mazingira ya kazi yao.

"Mnakutana na watu mbalimbali mnashiriki kwenye mikusanyiko, ni vyema mnapokwenda mfuate ushauri wa wataalam wetu wa afya, ili kujikinga," alisema.

"Tujitahidi kuendelea kunawa mikono au kutumia vitakasa mikono mara kwa mara, tunashikana mikono na watu wengi na wa aina mbalimbali kwa siku pia hata kuvaa barakoa ikibidi, itatusaidia kubaki salama," alisema.

Aliwahimiza kutumia kalamu zao kuelimisha jamii kuendelea kuchukua tahadhari kukabiliana na ugonjwa huo.

Alisema licha ya maambukizi ya ugonjwa huo kuwa chini hapa nchini, ni vyema wananchi wakaendelea kufuata ushauri wa watalaamu wa afya na iwe sehemu ya maisha yao.

Dk. Lutalala alisema tahadhari hizo zinatakiwa kuwa endelevu ili kujikinga kwa magonjwa mengine ya mlipuko kama kipindupindu.

"Katika kupambana na Corona tulisisitizwa sana usafi, unaponawa mikono yako kwa maji na sabuni unakuwa salama zaidi hata unapoenda kula chakula, hivyo inakuwa sehemu ya kujikinga na magonjwa yatokanayo na uchafu hivyo tuendelee na maisha hayo,"alisema.

Naye Mwandishi mkongwe, Noor Shija, aliwataka waandishi kutotumia maneno ambayo yataongeza hofu katika jamii wakati wa kuripoti taarifa za milipuko.

Aliwashauri waandishi wa habari kushirikiana kwa karibu na wataalamu wa sekta ya afya ili kupata taarifa na misamiati sahihi ya magonjwa ili kupeleka elimu sahihi kwa wasomaji.

Mwandishi wa gazeti la Jamvi la Habari, Dotto Kwilasa, alishukuru uwepo wa mafunzo hayo ambayo yatawasaidia kwenye utekelezaji wa majukumu yao.

**Tahadhari hizo zinatakiwa kuwa endelevu ili kujikinga kwa magonjwa mengine ya mlipuko kama kipindupindu.**





# Maabara inayopima zaidi ya vipimo 4,000 yaanza

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAABARA ya kisasa yenye uwezo wa kupima vipimo zaidi ya 4,000 kwa wakati mmoja imeanza kutumika katika Hospitali ya K's iliyopo jijini hapa na kuwa ya kwanza kufunguliwa katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Katibu wa hospitali hiyo, Julius Mhina, alithibitisha hayo wakati akizungumza na Nipashe kuhusu maabara hiyo inavyoweza kupima vipimo zaidi ya 4,000 kwa wakati mmoja ikilinganishwa na maabara nyingine.

Mhina alisema maabara hiyo inayofahamika kwa jina la Lancet, ilianza kutoa huduma katika nchi mbalimbali barani Afrika ikiwamo, Afrika Kusini, Kenya, Rwanda, Nigeria na sasa Tanzania.

**Lengo la maabara hiyo kuletwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini hasa katika Hospitali ya K's ni kuboresha na kutoa huduma za matibabu kwa uhakika na haraka.**

"Maabara ya kisasa ya Lancet imeanza kutoa huduma ya vipimo zaidi ya 4,000 kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na kwamba itasaidia kutoa majibu haraka ukilinganisha na ilivyokuwa awali ambapo watu walilazimika kusubiri majibu ya vipimo kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili," alisema Mhina.

"Tunataka kuokoa maisha ya watu hivyo tukaona ni muhimu kusogeza vipimo hivyo kwa mikoa yetu ili waondokane na adha ya kutumia muda mrefu kusubiri majibu ya vipimo vyao ambavyo husafirishwa hadi Hospitali ya Muhimbili na kisha kurudishwa tena," aliongeza Mhina.

Katika hatua nyingine Mhina alieleza furaha yake baada ya hospitali hiyo kuibuka mshindi wa utoaji huduma za afya kwenye maonyesho ya wakulima (Nanenane) yaliyohitimishwa jana katika viwanja vya John Mwakangale, jijini hapa.

Kwa upande wake, Meneja wa maabara hiyo, alisema kwa Tanzania kuna jumla ya maabara 12 katika mikoa sita.

Alisema lengo la maabara hiyo kuletwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini hasa katika Hospitali ya K's ni kuboresha na kutoa huduma za matibabu kwa uhakika na haraka.

Pia maabara hiyo ina uwezo wa kupima magonjwa ya ngozi na athari nyingine za kiafya zinazowakumba wakulima walioathiriwa na kemikali zinazopatikana kwenye pembejeo za kilimo.

Maabara hiyo ni mahusus kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa afya za binadamu kwa kuzingatia ubora na umakini.




Mkurugenzi wa Masoko wa kampuni ya Bia ya Serengeti, Mark Mugisha (katikati), akizungumza na waandishi habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya Serebuka inayolenga kuwafanya Watanzania kufurahia maisha kupitia bia ya Serengeti Lager na Serengeti Lite. Kushoto ni Meneja wa mipango kwa wateja, Lulu Kihwelo na Mkuu wa Kitengo cha Bia wa kampuni hiyo, Anitha Msangi. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Wajasiriamali wenye ulemavu wapewa mil. 70/-

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, imetoa Sh. milioni 70 zinazotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa kikundi cha wajasiriamali wenye ulemavu wilayani humo (Uwalemba) kwa ajili ya kukuza shughuli zao.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuwa fedha hizo ni utekelezaji wa sheria ya uwezeshaji wa makundi maalumu.

Alisema kwa mujibu wa sheria asilimia 10 ya mapato ya ndani ya kila halmashauri inatakiwa kukopeshwa kwa vikundi vya wajasiriamali wa makundi matatu ambayo ni asilimia nne wanawake, nne vijana na mbili watu wenye ulemavu. Mfune alisema, waliamua kukikopesha kikundi hicho baada ya kuridhishwa na kazi inazofanya ikiwamo uzalishaji wa sabuni za aina mbalimbali.

"Kwa kipindi hiki cha miezi mitatu halmashauri ya wilaya imetoa mikopo wa Sh. milioni 70 ili kukiwezesha kikundi cha Uwalemba ambacho kimejikita kwenye shughuli za ujasiriamali wa kutengeneza sabuni baada ya kuridhishwa na uchapakazi, lakini na uamini wao licha ya kuwa na ulemavu wanajitahidi," alisema Mfune.

Katibu wa Kikundi hicho, Ramadhan Shamte, alisema moja ya mikakati yao ni kuongeza uzalishaji wa sabuni kwa kutumia mitambo ya kisasa ambayo inarahisha kazi.

Alisema licha ya kupata mkopo huo, kikundi kinauhitaji mkubwa wa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda na maombi hayo yalifikishwa kwa uongozi wa halmashauri.

"Kikundi chetu kina jumla ya watu sita ambao tuna ulemavu wa aina mbalimbali tuliamua kuanzisha kiwanda cha kutengeneza sabuni ili kujikwamua kiuchumi kupitia juhudi zetu, serikali ilituona na kutowezesha mkopo wa milioni 70 ambao utatusaidia sana kuboresha huduma zetu," alisema Shamte.

# Wakulima wahamasishwa kutumia teknolojia umwagiliaji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKULIMA wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wamehamasishwa kutumia teknolojia ya umwagiliaji wa mazao kwa kutumia nishati ya umeme ili kuzalisha katika kipindi chote cha mwaka.

Msimamizi wa Taasisi ya Kilimo Trust Ofisi ya Mbeya, Robert Mwaluseke, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe, kuwa kilimo cha sasa kinahitaji teknolojia ya umwagiliaji ambacho kitasaidia kuwa na uhakika wa mavuno na kuuza kwa muda wowote atakaoamua.

Mwaluseke alisema ni asilimia tatu ya wakulima wanatumia kilimo cha umwagiliaji licha ya kwamba nchi imebarikiwa kuwa na vyanzo vingi vya maji na nishati mbalimbali za umeme ambazo zinatumika kwenye umwagiliaji.

"Shirika letu linawahamasisha wakulima kuachana na habari za kilimo cha kutegemea mvua ambayo hawana uhakika nayo na kuwasababishia hasara ya mazao yao badala yake sasa wawekeze kwenye kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia nishati ya umeme ambayo itaunganishwa na mitambo ili kuzalisha kwa wingi na kupata tija kupitia kilimo," alisema Mwaluseke.

Alisema licha ya Taasisi hiyo kuwahamasisha wakulima kutumia teknolojia ya umwagiliaji, lakini pia wanawasaidia kutafuta masoko, kuwapatia mbinu mbalimbali zitakazowawezesha kuongeza uzalishaji mazao na kuwandaa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ili kuzalisha kulingana na hali ya hewa.

Pia wanawaunganisha wakulima na wadau wa uuzaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo kwa kuhakikisha wanapatiwa kwa bei nafuu.

Alitoa ushauri kwa serikali kupitia Wizara ya Kilimo kusimamia vyema sera katika sekta hiyo kwa kutengeneza mazingira wezeshi kwa wakulima na wachakataji wa mazao badala ya kutoa makatazo ya mara kwa mara ambayo hayamsaidii mkulima kusonga mbele.

Alisema ili sekta hiyo iendelee kuwa mkombozi wa wananchi wengi hapa nchini, viongozi waangalie upya namna ya kusimamia na kutekeleza sera mbalimbali zilizoko kwenye kilimo kwa kutoa ushauri wa kitaalam wa namna ya kutekeleza matakwa.

"Tanzania tuna sera nzuri sana ya kilimo, lakini kuna tatizo katika usimamizi na utekelezaji wake baadhi ya watendaji wamejikita zaidi kwenye makatazo badala ya kutoa elimu na ushauri wa kitalaam kwa wakulima na wajasiriamali kwa kuwa lengo la serikali ni kuboresha maisha ya wananchi wake kupitia kilimo," alisema Mwaluseke.

Miongoni mwa wakulima, Dustan Bansekile, kutoka Wilaya ya Rungwe, alisema tatizo linalowasibu ni kutokuwapo kwa ushirikiano baina yao hasa wanapotaka kuuza mazao kwa kila mmoja kujiamulia bei na mahali pa kuuzia hali inayowapa nafasi walanguzi kujipangia bei.





# Shein ajivunia mafanikio viwanda, biashara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema serikali imepata mafanikio makubwa katika kuendeleza na kuimarisha sekta za viwanda na biashara Zanzibar.

Aliyasema hayo jana Ikulu mjini Zanzibar alipokutana na uongozi wa Wizara ya Biashara na Viwanda ilipowasilisha utekelezaji wa Mpango Kazi wa Mwaka 2019/20, na Mpango Kazi wa mwaka 2020/21.

Dk. Shein alisema katika kipindi cha awamu ya saba ya uongozi wake, juhudi kubwa zimefanywa katika kuimarisha sheria, sera na miongozo mbalimbali na kuimarisha miundombinu muhimu kwa ukuaji wa sekta ya biashara na viwanda.

Alisema misingi hiyo iliyojengwa ni vyema ikaendelezwa ili serikali ijayo ya awamu ya nane ianze utekelezaji wa mipango yake kwa kasi zaidi.

**Misingi hiyo iliyojengwa ni vyema ikaendelezwa ili serikali ijayo ya awamu ya nane ianze utekelezaji wa mipango yake kwa kasi zaidi.**

Dk. Shein alisema kuwa Wizara hiyo imepata mafanikio makubwa hasa katika kipindi hiki cha miaka mitano chini ya uongozi wa Waziri wa Wizara hiyo, Balozi Amina Salum Ali.

Alisema misingi ya biashara iliyoanzishwa imesaidia kukua na kuimarika kwa biashara huria Zanzibar na kuvifufua na kuviendeleza viwanda kikiwamo cha sukari kilichoko Mahonda na ongezeko la uzalishaji wa bidhaa ambazo umesaidia upatikaji wa huduma na usalama wa chakula.

Aidha, aliwapongeza wawekezaji wa ndani kwa kujenga ujasiri wa kuwekeza katika maeneo mapya ya biashara ndani na nje ya nchi katika sekta mbalimbali.

Kuhusu vikao vya kutathmini utekelezaji wa mpango kazi ambavyo vimekuwa vikifanyika katika kipindi chote cha uongozi wake, Dk. Shein alisema vikao hivyo (bango kitita) ambavyo ni vya mwisho katika muda wa uongozi wake, vimemsaidia kwa kiasi kikubwa kufuatilia utekelezaji wa mipango ya serikali katika wizara zake.

Naye Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Abdulhamid Yahya Mzee, alisema mikutano hiyo (Bango Kitita) imekuwa na msaada mkubwa katika wizara za serikali.

Waziri wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina, alisema wizara katika mwaka 2020/21 inatarajia kuyaendeleza na kuyapima maeneo ya viwanda ambapo Wizara hiyo inaandaa Mpango wa matumizi na upembuzi yakinifu kwa eneo la Dunga.

Pia alisema wizara inakusudia kuliandaa eneo la Nyamanzi na kuandaa matamasha mbalimbali ambapo wizara inakusudia kuliandaa kwa ajili ya ubia eneo hilo kwa hatua za awali kufanya tathmini ya kimazingira na kijamii (ESIA) pamoja na kulisafisha.

Kwa upande wa Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC), alisema limezindua mtambo mpya wa uzalishaji wa mafuta ya mikaratusi katika kiwanda cha mafuta ya Makonyo na Arki za mimea huko Wawi Pemba.

Alisema wizara kupitia shirika hilo, inatarajia kuanzisha kiwanda cha kusarifu mwani katika eneo la Chamanangwe Pemba kwa kushirikiana na wawekezaji kutoka Indonesia.

# Walimu waonywa ushabiki wa siasa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Walimu Zanzibar (ZATU) kimewaomba walimu na wanachama wake kutoshabikia vyama vya siasa wanapokuwa katika majukumu yao badala yake waitumikie jamii kwa haki na usawa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini hapa, Naibu Katibu Mkuu wa ZATU, Salim Ali, alisema katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu, hamasa ya wananchi huwa kubwa katika mambo ya siasa, hivyo kuna haja kwa kundi hilo kuhakikisha wanasimamia misingi ya taaluma yao, sheria na kanuni za utumishi wa umma ili kuepusha migongano na waajiri wao.

Salim alisema kuwa ZATU iliyoanzishwa miaka 25 iliyopita, haikatazi wanachama wake kujiunga au kugombea nafasi za uongozi katika vyama vya siasa bali inachowasisitiza ni kutochanganya masuala ya taaluma na siasa wakati wakitekeleza wajibu wao kwa jamii.

"Siku zote tumekuwa tukijifaharisha kuwa na viongozi wa kisiasa au serikali ambao ni walimu. Tunachokikataza ni walimu kufanya siasa wakiwa shuleni au maeneo yao ya kazi kwani ni kinyume cha sheria pia lina madhara makubwa kitaaluma kwa mwalimu na mwanafunzi," alisema.

Kuhusu utekelezaji na mafanikio ya kazi za chama hicho katika kipindi cha miaka miwili, Salim alisema kuna mafanikio mengi yaliyofikiwa na kuipongeza serikali kwa kuendelea kushirikiana nao kutatua changamoto za walimu na sekta ya elimu nchini.

Pia alipongeza juhudi zilizochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na wadau wa sekta ya afya kwa kukabiliana kikamilifu na maradhi ya corona ambayo yaliingia na kuathiri shughuli mbalimbali ikiwamo elimu.

"Chama chetu kinapongeza kwa dhati jinsi serikali ilivyotumia mapendekezo tuliyoyatoa katika kukabiliana na maradhi haya lakini pia walimu kwa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa kiwango cha elimu hakitoshuka," alisema.

**Siku zote tumekuwa tukijifaharisha kuwa na viongozi wa kisiasa au serikali ambao ni walimu. Tunachokikataza ni walimu kufanya siasa wakiwa shuleni au maeneo yao ya kazi.**



Mgombea Ubunge Jimbo la Gando Kisiwani Pemba kupitia Chama Cha Wananchi (CUF), Said Khalifa, akizungumza na waandishi wa habari juzi, baada ya chama chake kumpitisha kuwania nafasi hiyo, katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# RC ataka mabadiliko ya utendaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa Mjini Magharibi, Hassan Khatib Hassan, amewataka watendaji wa mabaraza ya manispaa kubadilika katika utendaji wa kazi ili kuondoa changamoto zinazoendelea kuukabili mkoa huo.

Alisema suala la ukusanyaji wa mapato na usafi wa mji si wa kuridhisha katika manispaa zote tatu za mkoa wa Mjini Magharibi jambo ambalo linapaswa kufanyiwa kazi kimkakati.

Aliyasema hayo jana alipokutana na viongozi wa manispaa na wilaya ofisini kwake Vuga, Zanzibar.

Alisema kuna mianya ya uvujaji wa mapato unaotokana na baadhi ya watumishi kutokuwa waaminifu jambo linalorudisha nyuma maendeleo ya manispaa hizo.

"Baadhi ya watumishi wenu si waaminifu, wamekuwa wakipoteza mapato hivyo nawaomba wakurugenzi wachukulieni hatua pale mtakapowabaini," alisema Hassan.

Kuhusu usafi wa jiji, Hassan alisema licha ya mabaraza hayo kutumia fedha nyingi kwa ajili ya usafi lakini bado ufanisi wake ni mdogo.

"Mnatumia fedha nyingi kwenye usafi lakini bado hali si nzuri. Tuna kazi ya ziada kuimarisha usafi wa maeneo yetu ili uendane na sifa za jiji," alisema Hassan.

Alisema wananchi wameitikia utaratibu wa uchangiaji wa uzoaji taka, lakini mabaraza hayo yanashindwa kuondoa taka kwenye madampo hali inayopelekea kuzagaa na kuondoa haiba ya jiji.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL,** Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile: **Kuboresha biashara, Kulipa kodi ya nyumba, Kumalizia tenda, Kulipa ada, Kulipa matibabu n.k.**
**Mawasiliano** yetu **Dar es salaam** – 0768 928 516. **Arusha** – 0677 226 960.

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi 88 /2020.**

**Ombi la NTULI MWAMBAPA MWAKIBETE kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi Marehemu FURAHA ANANGISYE MWAKIBETE**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 20/8/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

---

**RE: THE LAND ACT NO. 4 OF 1999**

**LOSS OF ORIGINAL LETTER OF OFFER**

**LOSS OF ORIGINAL LETTER OF OFFR OF;**

**REF: NO. L O N0 / S 195553**

**REGISTERED OWNER: JOYCE PYUZA**

**LAND: PLOT NO. 45 BLOCK 'JJ' LOCATION KIPONDODA**

**MANYONI DISTRICT**

**APPLICANT: JOYCE PYUZA**

**TAKE NOTICE** that the **ORIGINAL LETTER OF OFFER** to the land described above is said to be lost and that intend to issue a **REPLACEMENT OF ORIGINAL LETTER OF OFFER** in lieu therefore unless cause to the contrary is shown within thirty days from the date of this publication.
The **ORIGINAL LETTER OF OFFER** if found should be delivered to the office of the; District Director, Manyoni District Council, **P. O. BOX 60 Manyoni.**

Zamzam Hussein Seif
For: - DISTRICT DIRECTOR
MANYONI

---

**RE: THE LAND ACT NO. 4 OF 1999**

**LOSS OF ORIGINAL LETTER OF OFFER**

**LOSS OF ORIGINAL LETTER OF OFFR OF;**

**REF: NO. L O N0 / S 195561**

**REGISTERED OWNER: JOYCE PYUZA as the guardian of GOGLUCK JAMES (minor)**

**LAND: PLOT NO. 47 BLOCK 'JJ' LOCATION KIPONDODA**

**MANYONI DISTRICT**

**APPLICANT: JOYCE PYUZA**

**TAKE NOTICE** that the **ORIGINAL LETTER OF OFFER** to the land described above is said to be lost and that intend to issue a **REPLACEMENT OF ORIGINAL LETTER OF OFFER** in lieu therefore unless cause to the contrary is shown within thirty days from the date of this publication.

The **ORIGINAL LETTER OF OFFER** if found should be delivered to the office of the; District Director, Manyoni District Council, **P. O. BOX 60 Manyoni.**

Zamzam Hussein Seif
For: - DISTRICT DIRECTOR
MANYONI

---

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA KINONDONI**

**MIRATHI NA. 56 YA 2020**

**Maombi ya barua ya Usimamizi wa Mirathi ya Marehemu JAMES JOHN GONDWE**
**NA**
**JOHN ALLAN GONDWE WAOMBAJI/MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia Mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za Usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 20 mwezi 08 2020.
Imewasilishwa leo tarehe 06 mwezi 08 2020

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA KIVUKONI/KINONDONI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**SHERIA YA ARDHI NA.4 YA 1999**

**TANGAZO LA KUPOTELEWA KWA BARUA YA TOLEO LA ARDHI (LETTER OF OFFER)**

**KIWANJA NA. 10, KITALU 153 NGAMIANI TANGA**

TUNATOA TAARIFA YA KUPOTELEWA NKWA BARUA YA TOLEO LA ARHI YENYE NAMBA TAJWA HAPO JUU NA MAJINA YA ASBAT ABDIRAZAKI ABDALLAH NA HALIFA SAID SALEHE YEYOTE ATAKAYEIONA ANAOMBWA KUWASILIANA NA NAMBA ZA SIMU **0715309342**

---




**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Chanjo ya corona yaidhinishwa Urusi

**MOSCOW,** Urusi

RAIS wa Urusi, Vladimir Putin, amesema kwamba chanjo iliyotengenezwa nchini mwake kwa ajili ya ugonjwa wa corona, imeidhinishwa kwa matumizi baada ya kufanyiwa majaribio kwa binadamu katika kipindi cha miezi miwili.

Rais Putin amesema kwamba chanjo hiyo imepita vigezo vyote vilivyowekwa na kuongeza kwamba binti yake tayari amepatiwa na amepona.

Maofisa wa Urusi walisema kuwa wanampango wa kuanza kutoa chanjo hiyo kwa wananchi kuanzia Oktoba, mwaka huu. Wataalamu wameonesha wasiwasi wao kuhusu kasi ya kazi ya Urusi na kusema kuwa watafiti huenda wametumia njia za mkato.

**Wataalamu wameonesha wasiwasi wao kuhusu kasi ya kazi ya Urusi na kusema kuwa watafiti huenda wametumia njia za mkato.**

Huku wasiwasi ukiendelea kuhusu uwezekano wa usalama kuingiliwa wiki iliyopita, Shirika la Afya Duniani (WHO), liliitaka Urusi kufuata miongozo ya kimataifa ya kutengeneza chanjo dhidi ya virusi vya corona.

Chanjo iliyotengenzwa na Urusi sio miongoni mwa orodha ya zile za WHO ambazo zimefika awamu ya tatu ya majaribio kunakohusisha majaribio kwa watu wengi zaidi.

Akiitaja chanjo hiyo kuwa ya kwanza duniani, Rais Putin alisema chanjo iliyotengenezwa na taasisi ya Moscow ya Gamaleya, inatoa kinga endelevu dhidi ya virusi vya corona.

Waziri wa Afya wa Urusi, Mikhail Murashko, alisema chanjo hiyo imethibitisha kuwa salama na yenye ufanisi na kupongeza kwamba ni hatua kubwa kuelekea ushindi kwa mwanadamu dhidi ya ugonjwa wa corona.

Wiki iliyopita, Serikali ya Urusi ilitangaza kwamba inajitayarisha kuanza kutoa chanjo hiyo kwa umma, baada ya majaribio yake kufanikiwa.

Zaidi ya chanjo 100 kote duniani zinaendelea huku baadhi zikifanyiwa majaribio.Licha ya maendeleo hayo yaliyopigwa kwa haraka, wataalamu wengi wanafikiria kwamba chanjo hiyo haitakuwa inapatikana kwa wingi hadi katikati ya mwaka 2021.

Msemaji wa WHO, Christian Lindmeier, alisema baadhi ya watafiti binafsi wanadai wamebaini kitu, na bila shaka ni habari njema.

Alisema lakini katikati ya utafiti au kuwa na fununu ya kupata chanjo inayofanyakazi, na kupitia hatua zote, hatua kubwa imepigwa." **BBC**

# Kiongozi wa upinzani aikimbia nchi yake

**MINSK,** Belarus

KIONGOZI wa upinzani nchini Belarus, Svetlana Tikhanovskaya, anayepinga kuchaguliwa tena kwa Rais Alexander Lukashenko, amekimbilia nchini Lithuania.

Taarifa hiyo imetangazwa jana na Waziri wa Mambo ya nje wa Lithuania, Linas Linkevicius.

Tikhanouskaya mwenye umri wa miaka 37 aliibuka kuwa mpinzani mkuu wa Rais Lukashenko, akiwania uongozi baada ya mume wake kufungwa jela.

Linas Linkevicius alisema Svetlana, aliwasili Lithuania na yuko salama, huku maandamano dhidi ya ushindi wa Rais wa Belarus, aliyechaguliwa kwa muhula wa sita, yakiwa yametawanywa na polisi kwa usiku wa pili mfululizo.

Hayo yanajiri wakati Umoja wa Ulaya (EU) umetilia mashaka matokeo ya uchaguzi nchini humo.

Rais wa Halmashauri Kuu ya E, Ursula von der Leyen, aliitaka Belarus kutoa matokeo sahihi ya uchaguzi wa rais, baada ya Rais Alexander Lukashenko kuibuka na ushindi mkubwa.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, alieleza wasiwasi wake kuhusu hali nchini Belarus. Msemaji wake Stéphane Dujarric alisema kwamba Katibu Mkuu wa UN alitoa mwito kwa serikali kujizuwia na matumizi ya nguvu.

Rais Lukashenko alishinda uchaguzi wa Urais kwa asilimia 80 ya kura na kupongezwa na jirani yake, Rais wa Urusi, Vladmir Putin, lakini mataifa kadhaa ya Magharibi yameonyesha wasiwasi juu ya ushindi wake.

Awali Rais Lukashenko aliwaambia raia wa Taifa hilo kwamba hakutatokea vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Belarus, kwa kuwa amejipanga kuzuia majaribio yote ya kuidhoofisha serikali yake.

Usiku wa Jumatatu mamia ya raia waliandamana mjini Minsk ambako walijaribu kuweka vizuizi barabarani. **DW**



Rais wa Marekani, Donald Trump, akiondoshwa ghafla na maofisa usalama kwenye chumba cha mikutano, Ikulu mjini Washington DC. **PICHA: REUTERS**

# Ahukumiwa kifo baada ya kukufuru

**LAGOS,** Nigeria

MWANAMUZIKI Yahaya Sharif-Aminu, anayeishi katika jimbo la Kano lililopo Kaskazini mwa Nigeria, amehukumiwa kifo kwa kumkufuru Mtume Mohammad.

Mahakama ya juu ya kiislamu inayotumia sheria katika eneo la Hausawa Filin Hockey katika jimbo la Kano, imesema kuwa Yahaya Sharif-Aminu, mwenye umri wa miaka 22, alipatikana na hatia ya kukufuru kwa wimbo wake uliosambazwa kupitia mtandao wa WhatsApp Machi, mwaka huu.

Wakati wa kesi yake, Sharif-Aminu hakukanusha mashtaka yaliyokuwa yanamkabiri Jaji Khadi Aliyu Muhammad Kani alisema kuwa anaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo dhidi yake.

Majimbo ya kaskazini mwa Nigeria yanayokaliwa na Waislamu wengi hutumia sheria ya kiislamu na sheria ya kawaida, ambayo haitumiwi kwa watu ambao sio wafuasi wa dini ya kiislamu.



Ni moja tu ya hukumu za kifo iliyopitishwa na mahakama za sheria nchini Nigeria tangu zilipoanzishwa mwaka 1999.

Mwanamuziki huyo ambaye kwa sasa anashikiliwa mahabusu, alikua amejificha baada ya kutunga wimbo huo.

Waandamanaji walikua wamechoma moto nyumba ya familia yake na kukusanyika nje ya makao makuu ya polisi ya kiislamu huko Hisbah, wakidai hatua ichukuliwe dhidi yake.

Wakosoaji wanasema wimbo ulikufuru kwani ulimsifu imam kutoka Waislam wa Tijaniya kiasi kwamba ulimpatia hadhi ya juu kuliko Mtume Muhammad.

Wafuasi hao walikuwa wakisema kuwa hukumu iliyotolewa dhidi ya Yahaya itakua mfano kwa wengine.

Kiongozi wa maandamano ambayo yalidai kukamatwa kwa mwanamuziki huyo Machi, mwaka huu, Idris Ibrahim, alisema kuwa hukumu itakuwa kama onyo kwa wengine.

"Hukumu hii itakuwa ni onyo kwa wanaojaribu kufuata nyayo za Yahaya. Niliposikia kuhusu hukumu nilifurahi sana kwa sababu inaonesha kuwa maandamano yetu hayakua ya bure" alisema Ibrahim na kuongeza:

"Hukumu hii itakua ni mfano kwa wale ambao wanahisi kuwa wanaweza kutukana dini yetu au mtume na waendelee kuwa huru," alisema Ibrahim. **BBC**

# LIVERPOOL YAKAMILISHA USAJILI WA TSIMIKAS




**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL imethibitisha kumsajili mlinzi, Konstantinos Tsimikas kwa mkataba wa muda mrefu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ugiriki ambaye anacheza nafasi ya mlinzi wa kushoto, Tsimikas amejiunga na mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England kutoka Olympiacos kwa ada iliyoripotiwa kuwa pauni milioni 11.7.

Ujio wa nyota huyo mwenye umri wa miaka 24, umeongeza chaguo la ziada kwa Andy Robertson, ambapo kocha Jurgen Klopp alikuwa anatafuta mtu wa kumsaidia mlinzi huyo kwa msimu wa 2020-21.

Liverpool pia ilikuwa ikihusishwa na nyota wa Norwich City, Jamal Lewis, lakini ripoti zinasema kwamba walishindwa kufikia makubaliano na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ireland Kaskazini.

"Nina furaha kubwa, najisikia fahari kuwa hapa. Kwangu mimi hii ni klabu kubwa duniani," alisema Tsimikas akiiambia tovuti ya Liverpool.

"Ni heshima kubwa hapa na nitacheza kwa kiwango changu bora kabisa."

"Ligi ya hapa naipenda sana. Nimekuwa nikiifuatilia kwenye televisheni na nilikuwa na ndoto ya kuja kucheza hapa siku moja tangu nikiwa mdogo."

# Kocha aigusa Chelsea usajili wa Havertz

**DUSSELDORF,** Ujerumani

KOCHA Mkuu wa Bayer Leverkusen, Peter Bosz, ameitania Chelsea kwa mchezaji wanayemuwania, Kai Havertz, kwamba atajiunga na Heracles Almelo baada ya miamba hao wa Ujerumani kutolewa kwenye robo fainali ya Europa.

Mbio za Leverkusen kwenye mashindano hayo ya Ulaya zilifikia ukingoni Jumatatu, baada ya kuchapwa 2-0 na Inter Milan mjini Dusseldorf.

Mabao ya Nicolo Barella na Romelu Lukaku yakaipa Inter ushindi huo ndani ya dakika 21, kabla ya Havertz kupunguza moja dakika tatu baadaye.

Havertz amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka Leverkusen kwenda kwa miamba wa Ligi Kuu ya England, Chelsea, mara baada ya msimu huu wa 2019-20 kumalizika, na Bosz aliulizwa kama mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani amecheza mechi yake ya mwisho kwa klabu hiyo.

"Ndio, naweza kutangaza kwamba ataichezea Heracles Almelo ya Uholanzi," alisema Bosz, ambaye aliwahi kuinoa Heracles katika misimu miwili tofauti, akiwaambia waandishi wa habari.

Akizungumzia mchezo huo, Bosz alisema: "Tumepoteza dhidi ya timu kubwa. Hatukucheza vizuri katika dakika 20 za mwanzo na tulikuwa na tatizo la kumkaba Lukaku.

"Halafu akatuadhibu na tukashindwa kufanya lolote. Hivyo naamini kabisa kwamba tumepoteza kutokana na kuzidiwa nguvu."





# *Solskjaer sasa akataa kumzungumzia Sancho*

**COLOGNE,** Ujerumani

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, alikataa kuzungumzia kuhusu uvumi wa usajili wa mchezaji wanayemuwania, Jadon Sancho baada ya 'Mashetani Wekundu' hao kutinga nusu fainali ya Ligi ya Europa.

United ilitinga hatua hiyo baada ya kuibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Copenhagen ya Denmark katika muda wa ziada, Jumatatu.

Bao la penalti ya Bruno Fernandes ya dakika ya 95 liliwawezesha miamba hao wa Ligi Kuu ya England kutinga hatua hiyo na sasa wanasubiri mshindi kati ya Wolves na Sevilla.

Lakini wakati akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo, maswali mengi yalihusu nyota wanayemuwania kutoka Borussia Dortmund, Sancho.

Alipoulizwa kuhusu Sancho, Solskjaer alijibu: "Siwezi kumzungumzia mchezaji wa timu nyingine, siwezi kufanya hivyo. Mnajua hivyo. Siwezi kufanya."

Aidha, Solskjaer aliongeza: "Nina furaha tumefuzu. Nafikiri tulistahili ushindi huu usiku huu (juzi).

"Unaweza kuwa moja ya usiku bora zaidi kwetu, kwani mchezo ungeweza kumalizwa kwa mikwaju ya penalti, lakini tumefanikiwa kushinda."

## HABARI MICHEZO



# STURRIDGE ATAKA KURUDI EPL

**LONDON,** England

DANIEL Sturridge anataka kurudi Ligi Kuu ya England, kwani kazi aliyoianza bado hajaimaliza, kwa mujibu wa Sky Sports.

Straika huyo wa zamani wa England, amekuwa nje ya mchezo huo tangu alipoondoka kwa miamba wa Uturuki, Trabzonspor, Machi baada ya kufungiwa kwa miezi minne kwa kuvunja sheria ya kucheza kamari.

Lakini Sturridge aliendelea kujifua kwenye mazoezi mjini Los Angeles nchini Marekani na amesema yupo tayari kwa ajili ya kuendeleza kipaji chake katika ukurasa mpya.

"Kuna ofa nyingi kutoka kila sehemu duniani, lakini mimi ni mchezaji wa Uingereza na mara zote napenda kucheza kwenye Ligi Kuu ya England," alisema katika mahojiano maalumu na Sky Sport.

"Naamini nimepata mengi ya kuyatoa kwenye Ligi Kuu na naweza kucheza popote, lakini chaguo la kwanza ni EPL. Nahisi kama sijamaliza kazi niliyoianza kule na ningependa kurudi tena kule.

"Naweza kucheza kwenye ligi nyingine, lakini chaguo la kwanza ni Ligi Kuu ya England nataka kwenda kuonyesha tena ubora wangu.

"Kwa sasa nina njaa kubwa ya mafanikio kuliko hapo awali na kwa hakika kabisa nataka kuendelea kucheza."

Sturridge, ambaye anafikisha umri wa miaka 31 mwezi ujao, amefunga mabao 105 katika mechi 306 alizocheza kwenye Ligi kuu ya England wakati akiwa Manchester City, Chelsea, Bolton, Liverpool na West Brom.

## Barca yawania kumsajili Garcia kutoka Man City

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA itajaribu kumsajili tena mlinzi wa Manchester City, Eric Garcia kipindi hiki cha majira ya joto, lakini vyanzo zimeiambia ESPN kwamba klabu hiyo haipo tayari kulipa kiasi cha euro milioni 15 kwa mchezaji ambaye mkataba wake unamalizika msimu ujao.

Barca wangependa kumsajili Garcia kipindi hiki, lakini wanakabiliwa na vizingiti vingi ili kukamilisha dili hilo.


Bajeti yao ya usajili imekumbwa na changamoto baada ya mlipuko wa virusi vya corona na wataweza tu kuingia sokoni kama wakiuza nyota wake kadhaa, huku wakiwa na uwezekano wa kumuuza Samuel Umtiti na Jean-Clair Todibo.

ESPN kwa mara ya kwanza Juni 2, mwaka huu iliripoti nia ya Barca kumsajili tena Garcia, ambaye aliondoka klabuni hapo na kwenda Man City mwaka 2017.

City imejaribu mara kadhaa kumshawishi Garcia kusaini mkataba mpya, huku wa sasa ukimalizika mwaka 2021, lakini Pep Guardiola alithibitisha wiki iliyopita kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, amekataa.

Barca bado hajawasiliana na City kuhusu Garcia na inataka kufanya hivyo mara tu baada ya kumalizika kwa mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ambapo klabu zote zimetinga robo fainali.





## Ronaldinho anaweza kuachiwa Agosti 24

**ASUNCION,** Paraguay

RONALDINHO na kaka yake, Roberto de Assis, wanaweza kuachiwa huru kutoka kushikiliwa nchini Paraguay Agosti 24, mwaka huu, tarehe ambayo Jaji anatarajia kutolea uamuzi wa hukumu ya rufaa yao.

Jaji anayehusika na kesi hiyo, Gustavo Amarilla, alipanga tarehe hiyo kwa ajili ya kupitia makubaliano ya kuachiwa huru, Jumatatu.

Nyota huyo wa zamani wa Brazil na Barcelona na Roberto walikamatwa Machi, mwaka huu kwa kuingia nchini humo kwa kutumia hati ya kusafiria ya kughushi na walikaa jela kwa siku 32.

Mshindi huyo wa Ballon d'Or na kaka yake walilipa kila mmoja dhamana ya dola 800,000 na walipelekwa kwenye hoteli ya kifahari iliyopo katika mji mkuu wa nchi hiyo, Asuncion, na walibakia humo kwa amri ya kutotoka nje.

Na wamekuwa wakikaa kwenye hoteli hiyo hadi sasa na Ronaldinho mwenye umri wa miaka 40, na kaka yake wanaweza kuhukumiwa hadi miaka mitano jela kama wakikutwa na hatia.

Watetezi wao hivi karibuni walikubaliana na waendesha mashtaka kuwa wateja wao wanakosa kwa kuingia Paraguay kwa kutumia hati za kughushi na walitozwa faini ya dola 90,000 na 110,000, kwa Ronaldinho na Roberto.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# CONTE ACHAMBUA MAFANIKIO LUKAKU

**●●● Nina furaha juu yake, anastahili mafanikio yote haya, lakini lazima pia awashukuru...**

**DUSSELDORF,** Ujerumani

ANTONIO Conte amemsifia Romelu Lukaku baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia kwenye mchezo wa robo fainali ya Ligi ya Europa, lakini amesisitiza mafanikio ya mshambuliaji huyo yanatokana na mchango wa wachezaji wenzake wa Inter Milan.

Lukaku alifunga bao la ushindi kwa Inter na kuipeleka nusu fainali ya Kombe la Ligi ya Europa na sasa watacheza na kati ya Shakhtar Donetsk au Basel (waliocheza jana Jumanne), baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Bayer Leverkusen, Jumatatu.

Nicolo Barella alifunga bao la uongozi huku Lukaku mchezaji wa kimataifa wa Ubelgiji akifunga la pili na Kai Havertz akiwafungia la kufutia machozi Leverkusen.

**Lukaku angeweza kufunga hat-trick, baada ya mwamuzi Carlos del Cerro Grande kuzikataa penalti zake mbili kwa msaada wa VAR.**

Lakini wakati akimsifia Lukaku, ambaye amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga katika mechi tisa mfululizo kwenye Ligi ya Europa na akiwa amefunga mabao 29 katika mashindano yote msimu huu, Conte amebainisha mafanikio yake si chochote bila kupewa sapoti na wachezaji wenzake.

"Ni vigumu kumzunguzia mtu mmoja mmoja wakati unapokuwa na timu yenye kiwango kama hiki," alisema kocha huyo mkuu wa Inter, Conte akiiambia Sky Italia.

"Romelu yupo kwenye msimu wake bora kabisa, akisapotiwa na timu, ambayo inamfanya kila mmoja kuonyesha kiwango chake.

"Nina furaha juu yake, anastahili mafanikio yote haya, lakini Romelu lazima pia awashukuru wachezaji wenzake kwa kumtengenezea mazingira bora kwake."

Aidha, Conte alikubali kwamba, timu yake inatakiwa kujiimarisha zaidi kwa kiwango chake, ili kuweza kulibeba kombe hilo msimu huu.

Inter haijatwaa taji lolote la Ulaya tangu mwaka 2010 wakati ilipobeba lile la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Nimeridhishwa na kiwango, lakini bado tunatakiwa kuimarika na kuonyesha njaa zaidi ya mafanikio," alisema Conte.

## ZISIKUPITE

### PIRLO HAMTAKI RASMSEY

NYOTA Aaron Ramsey hatakiwi na kocha mpya wa Juventus, Andrea Pirlo na kiungo huyo mwenye umri wa miaka 29, raia wa Wales yupo huru kutafuta klabu nyingine. ***(Mirror)***

### UNITED WAPO NA SANCHO

MANCHESTER United itaendelea kumshawishi nyota wa England, Jadon Sancho, licha ya Borussia Dortmund kudai mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, atabakia klabuni hapo msimu ujao. ***(Mail)***

### INTER YAMTAKA SMALLING

INTER Milan inawania kumsajili mlinzi wa Manchester United, Chris Smalling mwenye umri wa miaka 30, ambaye alikuwa anacheza kwa mkopo pale Roma. ***(Gazzetta dello Sport)***

### MATUIDI KUTUA MIAMI

KIUNGO wa Juventus, Blaise Matuidi mwenye umri wamiaka 33, atajiunga na miamba wa Ligi Kuu ya Marekani (MLS), Inter Miami kama akifuzu vipimo vya afya. ***(Goal)***

### HAVERTZ APEWA MI5 CHELSEA

CHELSEA wamefikia makubaliano ya mkataba wa miaka mitano na mshambuliaji wa Bayer Leverkusen na Ujerumani, Kai Havertz, lakini nyota huyo mwenye umri wa miaka 21, atawagharimu pauni milioni 90. ***(RMC Sport, via Sun)***

### WILLIAN NJIA NYEUPE ARSENAL

ARSENAL wapo njia nyeupe kukamilisha usajili wa kiungo wa zamani wa Chelsea, Willian baada ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 32, raia wa Brazil kufuzu vipimo vya afya. ***(Standard)***

### SPURS YAMUWANIA RYAN

MLINZI wa kushoto wa Tottenham Hotspur, Ryan Sessegnon, mwenye umri wa miaka 20, anawaniwa na Newcastle United. ***(Sun)***

### AWINDWA CHELSEA, LAZIO

CHELSEA inakabiliwa na ushindani kutoka Lazio katika mbio za kuwania kumsajili mlinzi wa Real Madrid na Hispania, Sergio Reguilon mwenye umri wa miaka 23. ***(DiMarzio)***

### BAKAYOKO BEI POA CHELSEA

CHELSEA inajiandaa kushusha bei kwa kiungo wake wa Ufaransa, Tiemoue Bakayoko mwenye umri wa miaka 25. Klabu hiyo inatumaini watapata pauni milioni 20 kutoka kwa AC Milan ambao wanamuwania. ***(Sun)***

### LYON KUMUUZA TRAORE

KLABU ya Lyon inajiandaa kumuuza winga wa zamani wa Chelsea, Bertrand Traore kipindi hiki cha majira ya joto, huku Newcastle, Leicester, Everton na Crystal Palace zikimuwania nyota huyo wa kimataifa wa Burkina Faso mwenye umri wa miaka 24. ***(Sky Sports)***

### BUENDIA AWINDWA PALACE

ASTON Villa na Crystal Palace zinahusishwa na uhamisho wa kiungo wa Norwich na Argentina, Emiliano Buendia mwenye umri wa miaka 23. ***(HITC, via Sun)***

HABARI MICHEZO

## Buffalo wafufua matumaini Kriketi

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Buffalo Blasters imefufua matumaini ya kufanya vizuri katika ligi ya mchezo huo iitwayo APL kufuatia ushindi wa kishindo wa wiketi sita iliyoupata dhidi ya Chui Challengers katika mechi iliyochezwa jijini Dar es Salaam jana.

Ligi hiyo, ambayo hufanyika kila mwaka, inaandaliwa na Chama cha Mchezo wa Kriketi nchini (TCA) ikiwa na lengo la kuuendeleza mchezo huo.

Chui Challengers walipata fursa ya kuanza kupiga mpira, wakapata mikimbio 84 katika ova 18.2 huku wapigaji wao wote wakitolewa. Khalil Rehemtullah alikuwa na mchezo mzuri wakati wa fursa ya timu hiyo kupiga mpira kwani alipata mikimbio 29.

Abdullah Jabiri alikuwa mchezaji mwingine aliyeng'ara katika timu hiyo wakati wa fursa hiyo, akipata mikimbio 18. Goodluck Andrew, Salum Jumbe na Ankit Baghel walikuwa na mchezo mzuri wakati wa fursa ya Chui Challengers kurusha mpira, wakichukua wiketi mbili kila mmoja.

Buffalo Blasters hawakupata upinzani mkali wakati wakitafuta idadi ya mikimbio 85 waliyotakiwa kuipata ili washinde, wakiifikia idadi hiyo huku wakipoteza wiketi nne katika ova 16.

Ushindi wa jana ulikuwa ni wa kwanza kwa Buffalo Blasters katika ligi hiyo, inayochezwa katika viwanja vya Gymkhana, wakiwa wameshacheza mechi tatu baada ya kuanza kwa kupoteza wiketi tatu kwa Simba Kings katika mechi iliyochezwa Jumamosi iliyopita.

Buffalo Blasters kisha wakafungwa na Twiga Titans kwa mikimbio 48 katika mechi ya pili iliyochezwa Jumapili.

## Mashindano Kuogelea kufanyika Agosti 29

**Na Mwandishi Wetu**

Mashindano ya wazi ya Kuogelea ya HPT yanatarajiwa kufanyika Agosti 29, mwaka huu katika Bwawa la Shule ya Sekondari ya Shaaban Robert, Upanga jijini Dar es Salaam.

Katibu Mkuu wa Chama Cha Kuogelea Tanzania (TSA), Inviolata Itatiro, alisema jijini jana kuwa, mashindano hayo yameandaliwa na makocha wanaofundisha waogeleaji yajulikanayo kwa jina la High Performance Training na chama chao kuwapa kibali.

Inviolata alisema TSA inatambua mchango wa wadau katika kuendeleza mchezo huo hapa nchini na wanaamini mashindano hayo yatatoa picha halisi ya maendeleo ya waogeleaji baada ya kumpumzika kwa takribani miezi miwili na nusu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

"TSA inatambua mchango wa wadau katika kuhakikisha mchezo wa kuogelea unapata maendeleo. Hivyo mashindano ya wazi na mchanganyiko ya HPT ni ya kwanza tangu serikali kuruhusu michezo miezi miwili iliyopita," alisema Inviolata.

# ZAHERA RASMI MKURUGENZI WA UFUNDI GWAMBINA FC

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Gwambina FC, umeingia makubaliano na aliyekuwa Kocha wa Yanga, Mwinyi Zahera kuwa Mkurugezi wa ufundi wa timu hiyo iliyopanda Ligi Kuu msimu huu.

Akizungumza na gazeti jana, Katibu Mkuu wa Gwambina, Daniel Donald, alisema wameingia makubaliano ya muda mfupi na Zahera kuwa Mkurugezi wa ufundi na kama atakamilisha malengo na masharti waliyowekeana watampa mkataba wa muda mrefu.

"Mkataba huu ni wa muda mfupi, nafasi yake ni mkurugenzi wa ufundi na si kocha mkuu kama inavyodaiwa, benchi letu la ufundi litaendelea kubaki vile vile kwa kocha mkuu kuendelea kuwa Novartus Fulgence ," alisema Donald.

**Alisema ujio wa Zahera hautabadilisha lolote katika benchi lao ufundi kinafasi, zaidi ya kuongeza nguvu na kuimarisha timu yao hiyo hasa katika suala la ufundi.**

"Tuna imani na Zahera kwani tunajua utendaji wake, atasaidia benchi letu la ufundi kuwa imara zaidi kwa ajili ya mapambano ya Ligi Kuu," alisema katibu huyo.

Kuhusu usajili, alisema unaendelea na tayari wako katika majadiliano na baadhi ya wachezaji kutoka timu za Ligi Kuu na Daraja la Kwanza.

"Asilimia kubwa tunabaki na wachezaji wetu ambao walipandisha timu, pia tutasajili nyota nane kutoka timu za chini hatuwataki wale walioachwa Simba na Yanga," alisema Daniel.

Alisema suala la Kelvin Yondani na Juma Abdul hawana mpango na nyota hao kutokana na kutokuwapo katika mipango ya benchi lao la ufundi.




Kocha Mkuu wa zamani wa Klabu ya Yanga, Mkongomani Mwinyi Zahera (kushoto) akipokea mkataba kutoka kwa Mkurugenzi wa Gwambina FC, Alexander Mnyeti, baada ya kujiunga na klabu hiyo kama mkurugenzi wa ufundi. Gwambina ya Misungwi mkoani Mwanza, imepada Ligi Kuu Bara msimu huu. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Wachezaji 19 waondoka Coastal Union*

**Na Adam Fungamwango**

COASTAL Union ya Tanga itawakosa wachezaji wake 19 msimu ujao ambao waliitumikia klabu hiyo msimu wa 2019/20 na kufanya vema kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Taarifa ya Coastal Union kwa vyombo vya habari kupitia mtandao wao rasmi wa klabu ni kwamba msimu ujao haitokuwa na wachezaji 19 waliokuwapo msimu uliopita kwa sababu baadhi yao wametemwa na wengine wamekwenda kujiunga na klabu zingine za Ligi Kuu.

Taarifa hiyo imeeleza kuwa wachezaji 12 wameachwa na klabu hiyo, huku saba wakiondoka na kwenda kujiunga na klabu zingine.

Imewataja wachezaji walioachwa kuwa ni Hasaan Mangayaba, James Kahimba, Deogratius Antony, Deal Makonga, Ally Mbarouk 'Babu Ally', Mohamed Kijiko, Hamad Majimengi, Exavery Ching'eng'e, Mohamed Vuai 'Prince', Daud Aboud na Aboubakar Nyakalungu.

Aidha, taarifa hiyo ya Coastal Union imewataja wachezaji saba waliokwenda kujiunga na klabu zingine kuwa ni Bakari Mwamnyeto aliyejiunga na Yanga, Ibrahim Ally Ame, aliyetua kwa Mabingwa wa Soka nchini, Simba na Ayoub Lyanga aliyesajiliwa na Azam FC.

Wengine ni Muhsin Malima aliyekwenda kucheza soka la kulipwa nchini Serbia, Andrew Sinchimba ambaye aliyesajiliwa na Azam FC jumla baada ya kipindi chake cha kuichezea kwa mkopo kumalizika, Makiada Franco, aliyeondoka na kwenda kujiunga na Mbao FC iliyopo Daraja la Kwanza kwa sasa, na Sudi Dondola ambaye amejiunga na KMC.

Msimu uliopia Coastal ilishika nafasi ya saba baada ya kuvuna pointi 53, ikiwa ni moja ya misimu bora kabisa kwa timu hiyo kuwa nayo baada ya miaka mingi.

Micheze

Jumatano Agosti 12, 2020

Nipashe



Conte achambua mafanikio Lukaku

UKURASA 22

ULINZI MKALI TFF...



Polisi wakiwa wameimarisha ulinzi nje ya uzio wa ofisi za Shirikisho la Soka nchini (TFF), wakati kesi ya Yanga na kiungo wa timu hiyo, Bernard Morrison, ikiendelea katika ofisi hizo jana. Umati wa mashabiki wa soka umekuwa ukikusanyika nje ya uzio wa ofisi hizo wakitaka kujua hatima ya kesi hiyo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Yanga yakwama kumsajili Sure Boy*

●●● Azam yafunga ukurasa wa kumuuza, wenyewe wasema nafasi yake bado ipo Jangwani lakini kama...

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya Salum Abubakar 'Sure Boy' kuonyesha nia ya kujiunga na Yanga kuelekea msimu mpya, klabu hiyo imeshindwa kufika dau ambalo linatakiwa, hivyo Azam FC kutangaza kumuondoa rasmi sokoni kiungo huyo, imeelezwa.

**Awali Yanga ilituma maombi ya kumsajili kiungo huyo, lakini Azam FC ilijibu kuwa hauzwi badaa ya kuzungumza na Sure Boy ambaye alionyesha nia ya kuendelea kuitumikia klabu yake hiyo iliyomlea tangu akiwa kinda.**

Hata hivyo, baadaye Azam FC ilikaribisha ofa kutoka Yanga baada ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Abdulkarim Amin 'Popat', kueleza kuwa Sure Boy ameuomba uongozi aruhusiwe kuondoka kwenda kutafuta changamoto nyingine.

Lakini jana Popat aliweka wazi kuwa wamefunga rasmi uamuzi wa kumuuza Sure Boy baada ya Yanga iliyokuwa ikimhitaji kushindwa kufika dau wanalolihitaji.

"Tuliwataka kuleta ofa yao, awali wakaja na Sh. milioni 20, tukakataa, baadaye wakaja na Sh. milioni 35 tukakataa, hivyo tumemuondoa sokoni kwa sababu hakuna klabu ambayo imefika dau," alisema Popat bila kuweka wazi dau wanalohitaji ili kumwachia kiungo huyo ambaye ameonyesha mapenzi yake kwa Yanga.

Akizungumzia uamuzi huo, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema tatizo ni kwamba Azam haitaki kusema kiasi inachohitaji ili kumuuza zaidi wanapokwenda na ofa yao hukataliwa kuwa ni ndogo.

"Wao waseme wanahitaji kumuuza kwa bei gani, mwanzo tulionyesha nia ya kumhitaji wakatukatalia kabla ya baadaye kueleza wapo tayari tupeleke ofa, tukatoa ofa ya Sh. milioni 20, wakasema ni ndogo tuongeze, tukarudi na Sh. milioni 35, bado wamekataa na kusema ni ndogo.

"Tatizo hawataki kutuambia wanamuuza bei gani, tunasikia tu kupitia kwenye mitandao kuwa anauzwa Sh. milioni 70, lakini hilo hawajatuambia sisi zaidi ya kukataa ofa zetu kuwa ni ndogo," alisema Bumbuli.

Aidha, Bumbuli alisema Yanga bado inamhitaji mchezaji huyo na nafasi yake wamemtengea, lakini endapo hawatafikia makubaliano na Azam, basi watageukia kwingineko ili kuziba nafasi hiyo.

Tangu kufunguliwa kwa dirisha la usajili Agosti Mosi, mwaka huu, Yanga imekuwa sokoni kusaka kiungo mkabaji kuziba nafasi ya Papy Tshishimbi ambaye wameacha naye baada ya kushindwana katika makubaliano ya mkataba mpya.

Dirisha la usajili linatarajiwa kufungwa mwishoni mwa mwezi huu huku Ligi Kuu Bara msimu wa 2020/21 ikitarajiwa kuanza Septemba 6, mwaka huu.

## Morrison, Yanga nyaraka kuamua

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

BAADA ya mvutano wa siku mbili bila kupata suluhisho ya uhalali wa mkataba wa kiungo Mghana Bernard Morrison na klabu yake ya Yanga, hatimaye kesi hiyo itaamuliwa baada ya Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), kupitia nyaraka muhimu leo.

Katika kesi hiyo iliyoanza kusikilizwa juzi, Yanga inadai kuingia mkataba mpya wa miaka miwili na Morrison, wakati mchezaji huyo akiukana na kudai saini yake imeghushiwa, wakati huu akiwa tayari ametia saini mkataba wa kuitumikia Simba kwa msimu mpya.

Baada ya juzi kuahidi kutoa hukumu hiyo jana saa 8:00 mchana, ilishindikana lakini Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji wa TFF, Elias Mwanjala, alisema kesi hiyo inaendelea tena leo baada ya kushindwa kukamilika kwa sababu ya kutokamilika kwa nyaraka moja kwa pande zote mbili.

Akizungumza na waandishi wa habari Makao Makuu ya TFF, Mwanjala alisema kesi hiyo imefika katika hatua nzuri, lakini kutokana na kukosekana kwa nyaraka hizo wanalazimika kukutana tena leo saa 4:30 baada ya pande zote mbili kuahidi kuleta nyaraka hizo jana usiku, hivyo matarajio ya hukumu ni leo.

"Kesi hiyo inaendelea vizuri, hadi sasa hakuna mshindi pande zote ni 50/50, baada ya kupata nyaraka hizo, tutapokutana tutaimaliza," alisema Mwanjala.

Hata hivyo, kwa mujibu wa chanzo chetu cha ndani ya kamati hiyo, nyaraka zinazohitajika ni risiti ya benki zilitolewa baada ya Yanga kumuingizia Morrison fedha za usajili huo.



9 770856 541002 >